**Wapandishwa** kizimbani tuhuma wizi wa mbolea

UKURASA 3



RIPOTI MAALUM

**Ongezeko** la watu linavyotishia uhai Hifadhi Ngorongoro

UKURASA 4



Mbatia: Wapinzani kususa hakutoi majibu, bali 'tukomalie' meza moja

Ukurasa 12

Ukurasa 13

RAIS SAHLE – WORK ZEWDE

Mwanamama aliyekanyaga Tanzania juzi, amefungasha neema ushirikiano

siasa

JUMATANO JANUARI 27, 2021

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU

Ukurasa 14

Huyu ndiye Lucy Lameck

MWEZI JANUARI; MAMA MAJANGA SIASA AFRIKA

• Miaka 50 Amin kupindua • Miaka 20 kuuawa Kabila • Miaka 10 janga la Mubarak

Aliyekuwa Rais Idi Amin Dada. **PICHA: MTANDAO**

fakari na matokeo yake yalizaa Mwongozo wa TANU uliopitishwa na ukawa halisi ukisimamia shughuli muhimu za kisiasa na kiuchumi kitaifa.

Sababu ilikuwa kuhakikisha kuwa chama kinahusika kila mahali, ili maadui wasipenye kupitia njia za kirasimu, waunde vikundi, wasijitenge na uongozi kutoa mwanya wa njama dhidi yake.

Hivyo nguvu ya chama zikawa siyo tu kushika hatamu bungeni (kupitisha sheria), pia katika ulinzi wa nchi.

**RAIS KABILA**

Kumbukumbu ya kuuawa Rais Laurent Kabila nchini Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), Januari 16, mwaka 2001 ni tukio kubwa lingine.

Ni kuanzia wimbi la vita kuondoa utawala wa Rais Mobutu Seseseko, yeye akiwa mgonjwa ng'ambo (akafia Morocco) iliharibika kabisa.

Papaa Kabila anadaiwa kuuawa na watu wa karibu yake, kutokana na ugomvi uliozuka kati yake na serikali ya Rwanda, ambayo kwa sehemu kubwa ilimsaidia kuunganisha nguvu ya kuondoa utawala wa Mobutu.

Jeshi la Zaire (ikiitwa hivyo wakati huo) lilikuwa halina itikadi ya pamoja au kiongozi, ila Mobutu awepo hapo.

Kuuawa kwa Papaa Kabila kuliitumbukiza DRC na eneo la katikati ya Afrika vitani na vurugu za kisiasa, nchi za upande wa kusini zikipambana na vikosi vya Rwanda na washirika wao ndani ya DRC.

Mwisho wake, Rwanda na marafiki zake wakarudi nyuma, wakaishia kulinda maslahi yao. Ni hali ambayo kimsingi imedumu na hadi sasa makundi tofauti yanapambana baina yao na zaidi kupigana na jeshi la nchi linalotaka sheria.

**MISRI NAKO**

Ripoti za vyombo vya habari kuhusu aliyekuwa Rais wa Misri, marehemu Hosni Mubarak, alichukua utawala baada ya Rais Anwar Sadat kupigwa risasi na askari aliyekuwa akishiriki gwaride, vuguvugu lenye mzizi mwezi Januari na akafa tarehe 25 ya mwezi uliofuata, Februari.

INAENDELEA UK.12

# Nipashe

Jumatano Januari 27, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580473

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US

UHABA MAFUTA YA KULA

# Shehena nyingine yaja bandarini Dar

UKURASA 2





Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akizungumza na Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Venance Mabeyo, alipofika Ikulu, Zanzibar jana. **Habari Uk.5. PICHA: IKULU ZANZIBAR**

## Operesheni watoroshaji wa mifugo yatangazwa

UKURASA 3



## Waziri apigilia msumari magari kukaguliwa TBS

UKURASA 2

**MICHEZO** GOMES AKUNWA NA CHIKWENDE, KAHATA UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Shehena nyingine mafuta ya kula yaja

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Viwanda, Geoffrey Mwambe, amesema shehena nyingine ya mafuta ya kula inatarajiwa kuwasili nchini Februari 17, mwaka huu, huku akitishia kuwafutia leseni mawakala wa bidhaa hiyo watakaobainika kuuza kwa bei kubwa tofauti na iliyopo sokoni.

Waziri Mwambe alitoa kauli hiyo jana alipozungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma kuhusu hali ya upatikanaji wa mafuta ya kula nchini.

"Kwa sasa tuna mafuta ya kutosha, lakini hizi meli mbili za tani 21,800 na nyingine 26,450, yote yameshapakuliwa. Ukijumlisha na ambayo yapo, hatutarajii uhaba wa mafuta, kinachotarajiwa ni bei kuongezeka," alisema.

Aliwaagiza Wakurugenzi wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, kufanya kazi na waagizaji wa mafuta hayo, ili usambazaji ufanyike kwa usahihi.

"Kwa wale mawakala wakubwa, ninaomba nitoe onyo kabisa, bei ambazo zitakubaliwa kiwandani tunajua hadi bei ya mwisho, wakiuza bei kubwa kuliko ambayo kiwanda kimetoa na faida yao kulingana mwenendo wa soko, mimi nitawafutia leseni ya biashara.

"Mimi nitafuta kabisa leseni za biashara, na wale wauzaji wa jumla ndio hivyo hivyo, bei zao zinatakiwa ziendane na uhalisia wa kilichotoka kiwandani, ninawaagiza Tume ya Ushindani (FCC) kufuatilia kwa kina na kuhakikisha hizo bei zinakwenda vizuri," alisema.

Mwambe alisema kuna baadhi ya gharama zimepunguzwa kwa kuwahisha kupakua mzigo huo, hivyo hakuna sababu mafuta kuuzwa kwa bei juu tofauti na bei ya soko iliyopo.

"Meli moja inapakua mafuta kati ya siku tatu hadi tano, sasa wale wenye meli wenyewe wanamtoza mwenye mzigo kila siku ya kusubiri pale Dola za Marekani 20,000 kutokana na kuchelewa kupakua mzigo.

"Kwa meli inapozidi kukaa kusubiri kuitwa kushusha mafuta, ndiyo gharama kubwa zinaongezeka kumlipa mwenye meli," Mwambe alifafanua.

Alisema kuna wakati meli ya mafuta inakaa siku 25 na kusababisha kuwapo kwa gharama kubwa na mwagizaji huyo huingiza gharama hizo kwa mtumiaji wa mwisho ambaye ni mlaji.

Alisema kuwa kutokana na kuwapo kwa foleni ya meli za mafuta, serikali kwa sasa imeweka utaratibu wa kuwahi kupakua mzigo meli za mafuta ya kula ili kuepusha kuwapo uhaba wa mafuta nchini.

"Kutokana na hali halisi ya mafuta mtaani, niliongea na Waziri mwenzangu wa Ujenzi na Uchukuzi, tutengeneze utaratibu wa kutoa kipaumbele kwa meli kushusha mafuta, tulianza kutumia tangu Desemba mwaka jana na meli itakayofika Februari 17 itashusha Februari 20," alisema.

Waziri huyo alisema matumizi ya mafuta nchini kwa mwezi ni tani 30,000 na kwa sasa mafuta yapo ya kutosha ikizingatiwa uzalishaji wa ndani unafanya vizuri.

"Mafuta yapo isipokuwa bei walizonunulia zimepanda kule nje, ndiyo maana na hilo ongezeko (la bei), hatutarajii kwa sasa uhaba mafuta, ila tunatarajia 'kabei' kuongezeka kutokana na nchi zinazozalisha kushuka uzalishaji wake," alisema.

Alisema uhaba huo unatokana na uzalishaji wa mbegu za mafuta nchini, kutotosheleza mahitaji yaliyopo na kutoa wito kwa wakulima kuzalisha kwa wingi, ili nchi ijitosheleze kwa mafuta kwa kuwa fursa hiyo ipo.

"Tuna fursa kama nchi, ni fursa kubwa kama tukihamasisha kuzalisha mbegu za mafuta kwa wingi, na kuna utaratibu mpya tunataka kuweka wa mikataba kwa wakulima," alisema.

Alisema viwanda vikubwa 21 vilivyopo nchini, uwezo wake wa kuchakata mafuta ni asilimia 25 hadi 35 na vingi havina malighafi kutokana na uzalishaji mdogo.

"Kwa mwaka, vinachakata miezi michache vinafungwa, wakulima wana fursa ya kulima zaidi kulisha viwanda na kuna viwanda vingine vidogo 750 vina uwezo wa kuchakata asilimia 20 tu na mbegu zinaisha," alisema.

Waziri huyo alisema Taasisi ya Utafiti wa Mbegu (ASA) na Taasisi ya Kilimo (TARI), zimefanya utafiti na kutoa mbegu bora ambazo zina uwezo wa kutoa mafuta mengi.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akiweka shada la maua kwenye kaburi la aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum, Martha Umbulla, katika mazishi yaliyofanyika nyumbani kwa marehemu kijiji cha Dongombeshi, wilayani Mbulu, jana. **PICHA: OWM**

# Waziri apigilia msumari magari kukaguliwa TBS

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Geoffrey Mwambe, amesema kuanzia Machi mosi, mwaka huu hakuna gari kutoka nje ya nchi litakalosajiliwa na kupewa namba na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) bila ya kukaguliwa na kuwa na cheti cha ukaguzi kutoka Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

Aidha, amewataka Watanzania kuanza kutumia mfumo wa kisasa wa kuagiza magari kwa kutumia mawakala waliosajiliwa na wenye leseni za biashara ili kuepuka kuagiza gari lisilo na ubora na kulazimika kurudisha liliponunuliwa.

Waziri Mwambe alitoa kauli hiyo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa mfumo wa ukaguzi wa magari yaliyotumika kutoka nje ya nchi utakaoanza Machi Mosi, 2021 na ukaguzi wake utafanywa ndani ya nchi na shirika hilo.

Alisema ukaguzi huo awali ulikuwa ukifanyika nje ya nchi, lakini kwa sasa utafanyika ndani ya nchi na gharama zake zitapungua kutoka Dola za Marekani 150 hadi 140 kwa gari moja.

"Machi mosi tutaanza ukaguzi wa magari nchini na unafanywa na TBS, hapo mwanzo walikuwa wanakagua nje, nchi yetu sio ya kuweka vitu ambavyo havina ubora," alisema.

Alisema wakaguzi waliokuwapo wanne mikataba yao inakoma Februari 28, mwaka huu na serikali imejipanga kwa kujenga uwezo wa kutumia wakaguzi wa ndani na kupata faida na kudhibiti ubora.

"TBS wamepewa fedha na serikali na wameagiza mitambo mikubwa, magari yatakaguliwa na kutengenezwa hapa nchini kama likibainika kuwa na shida, hakuna gari itakayosajiliwa na TRA na kupewa namba bila kukaguliwa na TBS," alisema.

Kuhusu mawakala, Waziri Mwambe alisema wana uhusiano wa kibiashara na wauza magari kutoka nje ya nchi kutokana na kuagiza magari mara kwa mara, hivyo sio rahisi kuletewa gari lisilo na kiwango.

"Mfumo huu wa ukaguzi wa magari ndani ya nchi, utafanya vizuri sana kama tukitumia mawakala badala ya kuagiza sisi wenyewe kienyeji kupitia mitandao, na hapo utaondokana na risk ya kuagiza gari halafu ukalazimika kulipeleka karakana au kurudi lilipotoka," alisema.

Aliongeza: "Wakitumiwa mawakala waliosajiliwa na wenye leseni ina maana wanatambulika na serikali na wanalipa kodi, hivyo wanaweza kushtaki au kushtakiwa pale watakapoenda kinyume cha makubaliano yenu."

Kadhalika, aliitaka TBS kuingia mkataba na Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) na Mamlaka ya Ufundi Stadi Tanzania (VETA) ili kupata vijana watakaojengewa uwezo wa kuifanya kazi hiyo.

"Hii itasaidia kusambaza utaalamu kwa vijana wengi, hivyo kuwa na uhakika wa kazi kufanyika kwa ufanisi, nimeshamwagiza Mkurugenzi wa TBS kwamba aingie mkataba na VETA na DIT ili wale vijana wapewe nafasi ya kufanya kazi kama Interns na wale Wajerumani wanaoleta mashine za ukaguzi, hii itasaidia kujenga uwezo wetu wa ndani," alisisitiza.

Alitaja faida ya matumizi ya mfumo wa ukaguzi nchini fedha hizo sasa zitabaki nchini ambapo awali zilikuwa zinalipwa nje ya nchi.

"Sasa ukiangalia idadi ya magari yanayoagizwa kwa mwaka takribani 40,000 utaona kabisa kiasi kikubwa cha fedha ambacho nchi itapata, lakini teknolojia hii sasa itakuwapo nchini mwetu, tayari jozi 12 zimepatikana kwa ajili ya upimaji wa magari na kila jozi moja itapima gari kwa dakika 15 hivyo karakana zitapata kazi," alisema. Alisema kupitia utaratibu huo hakutakuwa na mawakala wa ukaguzi bali TBS itakagua yenyewe ndani ya bandari, hivyo kutochelewesha huduma za ukaguzi wa magari.

Akielezea namna walivyojipanga kuifanya kazi hiyo, Mkurugenzi wa Uthibiti Ubora kutoka TBS, Lazaro Msalanga, alisema sehemu kubwa ya manunuzi yamekamilika na mitambo na vifaa mbalimbali vinatarajiwa kuingia nchini Februari 15, mwaka huu.

"Vifaa hivi vitakuwa ni mobile na vingine vitasimikwa, upande wa wataalamu wanaohitajika kufanya kazi hiyo tayari wameshaarifiwa kuanzia juzi na wataanza kuripoti ili vifaa vikifika waanze kupewa mafunzo ili programu yetu ifanikiwe na ianze kwa wakati," alisema.

HABARI KITAIFA

# JPM kuzindua shamba la miti

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

RAIS Dk. John Magufuli anatarajiwa kuwa mgeni rasmi kwenye kuzindua shamba la miti leo katika eneo la Butengo Wilaya ya Chato mkoani Geita.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mkuu wa Mkoa wa Geita, Robert Gabriel, alisema shamba hilo ni miongoni mwa mashamba 23 ya serikali yanayosimamiwa na kuendelezwa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS).

Shamba hilo lilianzishwa kutoka sehemu ya eneo la msitu mkubwa wa Hifadhi ya Biharamulo-Kahama uliyohifadhiwa mwaka 1954 kwa tangazo la serikali namba 292 na ilifanyiwa marekebisho mwaka 1959 kwa tangazo la serikali namba 311.

Gabriel alisema shughuli za upandaji miti katika shamba hilo jipya zilianza mwaka wa fedha 2017/2018, likiwa na ukubwa wa hekta 69,000 (sawa na kilomita za mraba 690) na ni la pili kwa ukubwa baada ya shamba la miti Sao Hill lililopo Mafinga mkoani Iringa.

Shamba la miti Sao Hill lilianzishwa mwaka 1936 likiwa na ukubwa wa hekta 135,900 likijumuisha msitu wa asili wenye hekta 47,900 na eneo la upandaji miti takribani hekta 88,000.

Alisema uanzishwaji na utekelezaji wa shamba hilo unakwendana sambamba na malengo ya serikali ya kuhifadhi mazingira na kuinua uchumi wa nchi na wananchi.

Aidha, alisema mradi huo mkubwa wa upandaji miti ambao serikali inawekeza katika misitu huo, unatarajiwa kutoa mchango mkubwa katika masuala mbalimbali kama kuhifadhi mazingira na kuchangia uhifadhi wa misitu katika kanda ya ziwa na nchi kwa ujumla, kuzalisha malighafi ya viwanda vya mazao ya misitu kama mbao, nguzo, karatasi na nishati, kutoa ajira kwa Watanzania hususan wa maeneo yanayozunguka shamba hilo na kujenga misingi ya uhifadhi kwa wananchi.

Pia kushirikishwa katika miradi mbalimbali ya upandaji miti katika maeneo yao na ufugaji wa nyuki na kutoa fursa ya kufanya kilimo mseto ili kuondoa umaskini na upungufu wa chakula kwa jamii.

Alisema kwa kutambua umuhimu wa mradi huo mkubwa kwa taifa, Rais Magufuli ameridhia kuzindua mradi huo kwa upandaji miti utaodumu kwa kizazi cha sasa na baadaye.

Uzinduzi huo unatarajiwa kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali toka ndani na nje ya mkoa wa Geita.

Gabriel alisema Rais Magufuli baada ya kuzindua shamba la miti ataelekea Wilaya ya Mbogwe, ambapo atembelea Kituo cha Afya Masumbwe.

# Msako watuhumiwa 67 utoroshaji mifugo waja

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Mifugo, ameliagiza Jeshi la Polisi kupitia Kikosi cha Kuzuia Wizi wa Mifugo, kuwakamata watuhumiwa 67 wa utoroshaji wa mifugo na mazao yake katika mipaka mbalimbali nchini ikiwamo Horohoro mkoani Tanga.

Mashimba Ndaki alitoa agizo hilo jana jijini Dodoma baada ya kupokea ripoti ya uchunguzi kuhusu utoroshaji wa mifugo mipakani, ikibainisha utoroshaji wa mifugo na mazao yake kwenda nchi za jirani.

"Waanze kukamatwa kuanzia leo (jana) hawa watoroshaji wa mifugo na wakamatwe mara moja, tuanze na hawa 67 ambao wanajulikana walipo," alisema.

Alisema serikali haiwezi kuvumilia uwapo wa watu wenye nia ovu kwa kutorosha rasilimali za nchi.

Aliwaonya wafanyabiashara ambao wanajihusisha na utoroshaji wa mifugo na mazao yake, waanze kutafuta kazi nyingine ya kufanya kwa kuwa wizara haitavumilia mtu yeyote atakayejihusisha na vitendo hivyo.

Waziri huyo alimwagiza Katibu wa Wizara hiyo anayeshughulikia Mifugo, Prof. Elisante Ole Gabriel, kuchambua ripoti hiyo na kuainisha mapendekezo yaliyotolewa ili sekta ya mifugo iwe na mchango mkubwa kwa pato la taifa.

"Pia, ushirikiano kati ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) uimarishwe ili kutatua kero zinazowakabili wafugaji, mifugo isikae muda mrefu wakati wa kusafirishwa kwenda sokoni," aliagiza.

Akizungumzia kuhusu urasimu na utoaji wa vibali, Ndaki aliwataka watumishi wa wizara waliopo kwenye minada ya upili na mipakani, kuacha urasimu wa kuchelewesha kutoa vibali.

"Ninaagiza nipatiwe orodha ya watumishi na viongozi wao na muda walioto huduma katika ofisi za minada ili kuwachukulia hatua za kinidhamu watakaobainika kwenda kinyume cha utaratibu wa kazi.

"Ninataka nipatiwe taarifa za watu hao kuanzia vyeo vyao, umri wao na muda waliohudumu kwenye minada husika, ili kuboresha kwenye eneo kwa sababu utaratibu wa kufanya kazi kwa mazoea umeshapitwa na wakati," aliagiza.

Awali, akisoma ripoti ya uchunguzi kuhusu utoroshaji wa mifugo mipakani, Kamishna Msaidizi wa Jeshi la Polisi Julius Mjengi, alisema kabla ya Novemba 7 mwaka jana, mifugo iliyokuwa inatoka kwenye minada ya awali ya Handeni na Kilindi kuelekea Kenya kupitia Mpaka wa Horohoro, haikuwa inafuata taratibu za forodha kama shehena nyingine.

Alibainisha kuwa takwimu za daftari la mifugo katika Mpaka wa Horohoro zinaonyesha idadi ya mifugo iliyopitishwa kuelekea Kenya kwa kipindi cha miaka 17 kutoka mwaka 2003 hadi Novemba mwaka jana, ilikuwa ni ng'ombe 24,980, mbuzi na kondoo 9,368 sawa na wastani wa ng'ombe 122 na mbuzi au kondoo 46 kwa mwezi.

"Baada ya uchunguzi, ilionekana kuwa kati ya Novemba 7, 2020 hadi Desemba 9, 2020, jumla ya ng'ombe 1,096, mbuzi na kondoo 1,044 walipitishwa katika Kituo cha Forodha kuelekea Kenya," alisema.

Alisema huo wastani wa idadi ya mifugo iliyopita mpakani ndani ya mwezi mmoja kulinganisha na siku za nyuma na hivyo kubaini viashiria vya udanganyifu wa kurekodi idadi sahihi ya mifugo inayokaguliwa kwenda Kenya hususani kwenye mpaka huo.

# Kizimbani tuhuma wizi wa mbolea



Baadhi ya watuhumiwa tisa wa kosa la wizi wa kilo 8,184 za mbolea aina ya Amoniam Naitreti yenye thamani ya Sh. milioni 17 mali ya kampuni ya ORICA, wakiwa chini ya ulinzi wa askari polisi, kabla ya kusomewa mashtaka yao katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: JUMANNE JUMA.**

**Na Hellen Mwango**

WAKAZI tisa wamesomewa mashtaka katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam, ikiwamo wizi wa kilo 8,184 za mbolea aina ya Amoniam Naitreti yenye thamani ya Sh. milioni 17 mali ya Kampuni ya ORICA, iliyokuwa ikisafirishwa kutoka Dar es Salaam kwenda Zambia.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Bashiru Mfinanga, Siliak Waipopo, Juma Waziri, Juma Salehe, Zakaria Ndaya, Abasi Sikanyika, God Mshana, Masumbuko Fumbo na Zefania Kigola.

Washtakiwa walisomewa mashtaka yao mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Yusto Luboroga, aliyepangiwa kusikiliza kesi hiyo.

Wakili wa Serikali, Neema Mushi, alidai kila mshtakiwa anakabiliwa na shtaka lake na kwamba kesi hiyo ina mashtaka tisa.

Mushi alidai shtaka la kwanza, Oktoba 26, 2020 katika Wilaya ya Tunduma, Mkoa wa Songwe, mshtakiwa wa kwanza mpaka wa tano, Mfinanga, Waipopo, Waziri, Ndaya na Saleh, waliiba jumla ya kilo 8,184 mbolea yenye thamani ya Sh. milioni 16.854 iliyokuwa ikisafirishwa kutoka jijini Dar es Salaam kwenda Zambia.

Ilidaiwa katika shtaka la sita mpaka la tisa, mshtakiwa wa sita mpaka wa tisa, Desemba 12, 2020 katika Wilaya ya Tunduma mkoani Songwe, washtakiwa Sikanyika, Mshana, Fumbo na Kigola walikutwa na mali ya wizi ikiwamo mbolea aina ya Amoniam Naitreti Kilo 778.65, mali ya kampuni hiyo iliyokuwa ikisafirishwa kutoka Dar es Salaam kwenda Zambia.

Upande wa Jamhuri ulidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika na uliomba mahakama kupanga tarehe ya kutajwa.


## TANGAZO

### MRADI WA UWEZESHAJI WAJASIRIAMALI WA KUBANGUA KOROSHO

Kampuni ya Kamal ya Jijini Dar es Salaam inayo furaha kuujulisha umma wa Watanzania kuwa imeanzisha mpango wa uwezeshaji wa wajasiriamali Watanzania ili wamiliki viwanda vya kubangua korosho.

Kama iliyotangazwa kwenye vyombo vya habari hivi karibuni, Kampuni ya Kamal, kwa kushirikiana na Taasisi za fedha, imeanzisha mpango ambao utawawezesha wajasiriamali Watanzania kumiliki viwanda vidogo vidogo vya kubangua korosho.

**Vigezo vya msingi**

- Mjasiriamali anayehitaji kuwa sehemu ya mradi huu wa kimapinduzi ya viwanda nchini atahitaji kuchangia asilimia 20 tu ambazo ni sawa na Shilingi milioni 16.92 tu.

NB: Kwa awamu hii ya kwanza, watahitajika wajasiriamali 100 Watanzania.

Kwa wale watakaokuwa tayari kushiriki katika mradi huu, wanatakiwa kutuma maombi yao kupitia **https://kamal-group.co.tz/** na soma zaidi kuhusu mpango huu kwenye tovuti yetu. *Wahi tujenge uchumi wa Viwanda!*

Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **15/02/2021.**

Waliochaguliwa wataarifiwa kwa njia ya barua pepe au simu mahali na tarehe ya kikao kitakachokuwepo week ya kwanza March 2021.

**Kwa maelezo zaidi, piga simu au WhatsApp: 0742308439**

RIPOTI MAALUM

# Ongezeko la watu linavyotishia uhai Hifadhi ya Ngorongoro - 2

**Katika toleo la jana, tuliona ongezeko la watu kwa zaidi ya asilimia 1,000, mifugo na shughuli za kibinadamu linavyoathiri uhai wa Ngorongoro huku umaskini na kiwango cha kutojua kusoma na kuandika cha asilimia 64.5 kilichopo na uwapo wa magugu vamizi. Endelea kufuatilia ripoti ya uchunguzi wa Nipashe:**

**Na Salome Kitomari,** aliyekuwa NGORONGORO

OFISA Mwandamizi wa Uhifadhi, Dk. Elibariki Bajuta, anasema Baraza la Wafugaji lilianzishwa mwaka 2000 likiwa na wajibu wa kuibua miradi ya jamii kwenye hifadhi, huku wajibu mkubwa wa Ngorongoro ukiwa ni kuwaendeleza kielimu, kiafya, maji na mifugo yao ambayo ndiyo kazi yao kubwa.

Baraza hilo pia lina wajibu wa kusimamia miradi ya elimu kwa kuwa wanapewa fedha za kusomesha wanafunzi na anaamini akielimika anaenda Arusha kuliko wakiwaacha ndani ya hifadhi na kwa kufanya hivyo, wanapunguza idadi ya watu.

Dk. Bajuta anasema pia wanasaidia kuhakikisha miradi inatunzwa, kuwa na mawasiliano baina ya jamii na mamlaka.

"Ni eneo dogo lililopewa hadhi tatu kidunia; ya kwanza ilitolewa Hifadhi ya Taifa Serengeti mwaka 1979 kuwa ni eneo la urithi wa duniani kutokana na baionuwai iliyopo, maliasili na vivutio vilivyopo, mwaka 2010 ilitambuliwa kama eneo la urithi mchanganyiko ambalo unaweza kupata taarifa mbalimbali mfano eneo la Oldvai George ambalo ni pekee duniani, unaweza kupata historia ya binadamu wa kale.

"Kuna eneo la Laitol ndiyo pekee duniani lenye ushahidi kuonyesha binadamu alianza kutembea na miguu miwili na ndiko kuna ushahidi wa nyayo, pamoja na maeneo ya uhifadhi na jamii kwa ujumla," anafafanua.

Anasema hadhi nyingine ilitolewa Aprili 18 mwaka 2018 ikitambulika na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO), kama eneo la utalii wa miamba na sura za nchi Geopark, eneo pekee Kusini mwa Jangwa la Sahara na ya kwanza nchini, ikisababishwa na maeneo yaliyoko ndani ya hifadhi na pembezoni kama Mlima Oldonyo Lengai na mchanga unaohama kwa takribani mita 17 kwa mwaka.

Maeneo mengine ya Geopark ni miinuko na mabonde kama kreta ya Ngorongoro, Almoti, Embakai na maeneo ya maji moto ya Easi na Engaruka.

"Hadhi hizi tatu zimeifanya Ngorongoro kuwa muhimu kidunia, ni eneo pekee ambalo UNESCO kulipa hadhi tatu inaonyesha umuhimu wa Ngorongoro kitaifa na kimataifa.

"Lengo kuu la Ngorongoro ni kuhakikisha majukumu ya uhifadhi, utalii na kuendeleza wananchi waliomo yanawekwa katika usawa, bila hivyo eneo hilo litabaki historia," anaonya.



Baadhi ya makazi ya wananchi wanaoishi ndani ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), kutokana na ongezeko la watu na mabadiliko mbalimbali wameanza kujenga nyumba za bati na kuachana na nyumba za asili. Eneo hilo kwa sasa limeelemewa na watu kutoka 8,000 mwaka 1959 hadi 200,000 pamoja na mifugo. **PICHA: SALOME KITOMARI, NGORONGORO**

**MUUNDO WA NGORONGORO**

Dk. Bajuta anasema mfumo wa usimamizi wa eneo hilo uko chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii, ambayo kuna Waziri, Katibu Mkuu na Bodi pamoja na Kamishna wa Hifadhi na wasaidizi wawili na kote kuna idara zilizo chini yao na kubwa ni Kurugenzi ya Maendeleo ya Jamii na Utalii.

Anasema Ngorongoro imepata mafanikio makubwa ya uhifadhi na utalii ambayo ni juhudi za serikali kuhakikisha inaendelea kuwapo.

"Mapato yameongezeka kwa kiwango kikubwa 2014/15 walikusanya Sh. bilioni 60 na mwaka 2018/19 walikusanya Sh. bilioni 143, huku mwaka 2019/20, licha ya corona walikusanya Sh. bilioni 122, ni mafanikio makubwa sana tuliyoyapata," anasema.

Anasema kuongezeka kwa mapato kuna maana kubwa katika kuchangia pato la taifa na imekuwa ni kati ya taasisi tano bora za serikali zinazotoa gawio kwa serikali na mwaka 2017/18 walichangia Sh. bilioni 18 ambayo ni asilimia 15.

Anasema mwaka 2018/19 walitoa gawio la Sh. bilioni 23 ikiwa ni mafanikio makubwa, na kwamba mwaka 2019/20 pamoja na corona walitoa gawio la Sh. bilioni 15.

Kwa upande wa utalii, pamoja na mapato kuongezeka, idadi ya wageni haikuwa nzuri na sababu kubwa ni mifumo thabiti ya ukusanyaji mapato na juhudi za mamlaka kukusanya mapato.

Anasema kuanzia mwezi Machi hadi Aprili mwaka jana, hakukua na mgeni hata mmoja kutokana na janga la corona na hawakukusanya fedha yoyote bali walitumia muda huo kuboresha miundombinu ya barabara, majengo na utalii kwa ujumla.

"Tumejenga jengo la kitega uchumi jijini Arusha ambalo linasaidia watalii kupata taarifa mbalimbali, huku wakiboresha mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato, uendeshaji wa shirika na bajeti," anasema.

Hifadhi hiyo ina ukubwa wa kilomita za mraba 11,895 kwa sasa ina watu zaidi ya 200,000 kutoka 8,000 wa mwaka 1959 likitapakaa katika wilaya za Karatu (Mang'ola na Eyasi) na Monduli (Enfaruka, Selela, Mlima Oldonyo Lengai na Engaresero).

Upande wa kaskazini umepakana na pori la akiba la Loliondo, magharibi na kaskazini magharibi imepakana na Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, Kaskazini-Mashariki inapakana na Ziwa Natron, Mashariki hadi Kusini Magharibi inapakana na Pori la Akiba la Maswa.

**BARAZA LA WAFUGAJI**

Wananchi wanaoishi ndani ya Ngorongoro, wanasema timu ya wataalamu iliyofanya mahojiano katika eneo hilo, haikusikiliza wenyeji wote, huku wakiomba nafasi ya kusikilizwa juu ya namna ya kusimamia eneo hilo.

Katika tamko lao la hivi karibuni, madiwani 11 wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro, vijiji 25 na kiongozi wa kimila wa tarafa ya Ngorongoro, James Moringe, anasema mapendekezo ya kutwaliwa kwa maeneo ya wenyeji siyo sahihi kwa kuwa itawaathiri kimaisha.

Moringe ambaye ni Diwani wa Kata ya Laitole (CCM), alieleza: "Sisi madiwani na Malaigwanani, kwa niaba ya wenyeji wa eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, kwa unyenyekevu tunamuomba ripoti hiyo isipokelewe, kuwe na ufuatiliaji wa kina wa uhusiano wa jamii na mamlaka.

Kabla ya kutolewa tamko hilo, Diwani wa Kakesio (CCM), Johannes Tiamasi, ambaye pia ni Katibu wa Baraza la Wafugaji nchini, alisisitiza kuwa wenyeji wako tayari kushirikiana na mamlaka kutatua matatizo ya mimea vamizi, ongezeko la idadi ya watu na maendeleo hafifu ya wenyeji.

"Shughuli za uhifadhi na za utalii zinachangia kwa sehemu kubwa kukuza uchumi wa nchi yetu na hivyo kupunguza umaskini. Wenyeji ni wahifadhi wa asili na wameendelea kuisaidia serikali katika kulinda, kutangaza na kushiriki kutatua matatizo yanayoikumba sekta ya maliasili na utalii," anasema Tiamasi.

**MUUNDO WA BARAZA**

Dk. Bajuta anasema lengo la kuwapo kwa baraza la wafugaji ni kuwa kiungo katika ya jamii na uhifadhi ili kurahisisha uhifadhi na kwamba miaka ya zamani kulikuwa na ujangili mkubwa na baraza likaja kama sehmu ya kuwasemea wananchi na kulinda uhifadhi.

"Katiba yao wanatengeneza wenyewe na wajumbe wake ni madiwani wote walioko ndani ya hifadhi, Wenyeviti wa vijiji, wawakilishi wa vijana, wanawake na wazee wa kimila wa vijiji 11 vilivyopo kwenye hifadhi," anabainisha.

"Utekelezaji wa mambo yanayofanywa na jamii ni kati ya baraza na vijiji, kama kuna misaada imetolewa kwa jamii haijafika wasemaji wa vijiji ni baraza, ila fedha zinapelekwa moja kwa moja kwenye vijiji, kinachobaki baraza ni uendeshaji...serikali imeshatoa maelekezo fedha za miradi ziende moja kwa moja halmashauri," anabainisha.

**WALIWAHI KUHAMISHA**

Kwa mujibu wa Dk. Bajuta, kaya 119 za watu zaidi ya 500 zilihamishwa eneo la Jema lililomegwa kutoka Oldonyosambu, lakini kaya nne zilirudi, lengo lilikuwa ni kupunguza idadi ya watu.

Anasema asilimia 20 wanamiliki asilimia 80 ya mifugo, huku hawaruhusiwi kufanya shughuli yoyote ya kilimo zaidi ya ufugaji, na asilimia kubwa ni maskini kwa kuwa hawana mifugo.

"Kama mamlaka baada ya kuona hali ilivyo na umaskini uliopo ndiyo maana tukapitia upya sheria iliyounda Ngorongoro na imeshafikia mahali pazuri pa namna ya kusonga mbele kwa manufaa endelevu ya matumizi mseto," anasema.

Kuhusu ugawaji wa chakula, anasema wamekuwa wakiwapa magunia 10 kwa mwaka, lakini kwa sasa hali siyo nzuri na wamesitisha kutoa chakula hicho na wanawahamasisha watoke nje ya hifadhi ili wakafanye shughuli za kilimo.

Anasema kamati ya serikali ndiyo itakuja na jibu la namna ya kusonga mbele kwa miaka 100 ijayo, kwa kuwa bila kufanya hivyo hali si njema kwa kuwa licha ya wengi kusomeshwa bado wamerudi hifadhini na hakuna namna ya kuwazuia wasirudi kwenye makazi yao ya asili.

HABARI KITAIFA

## Wadai kakakuona ametabiri neema

**Na Idda Mushi, MVOMERO**

MNYAMA jamii ya kakakuona ameibuka kwenye kituo cha kufundisha matengenezo ya umeme bila kuzima, kilichopo Kitongoji cha Wami Ranchi, Kata ya Wami Sokoine wilayani Mvomero mkoani Morogoro.

Kutokana na hali hiyo, viongozi wa dini na wa kimila, walishiriki kumwekea vitu mbalimbali zikiwamo silaha za jadi na vyakula kama unga, mahindi, mchele, maji na maziwa na vifaa vya matengenezo ya umeme ili atabiri.

Mnyama huyo aliyewekwa katikati ya vitu hivyo, alipita katikati ya unga na maziwa, kitendo kilichotajwa na viongozi wa dini akiwamo Sheikh Yahya Kilo na kiongozi wa kimila wa kabila la Wamasai ambao wengi ndio wenyeji wa kijiji hicho na baadhi waliofika kushuhudia, Mchungaji Msendekwa Ndese, wakasema kitendo hicho kimeonyesha neema kubwa ya upatikanaji wa chakula msimu huu, kupitia sekta ya kilimo na mifugo.

"Mnyama huyu amewekwa huru, katikati ya vitu vingi, akageuka kushoto na kulia na kuamua kuchagua chakula. Kwanza niliogopa nikaona ameelekeza macho kwenye mshale, lakini akageuka na kufuata maziwa na unga, ametupa faraja kubwa kuona tuna neema ya chakula," alisema Mch. Ndesse aliyefika katika kituo hicho cha kutengeneza umeme bila kuzima, akiwa na gari aina ya Harrier nyeusi.

Ndese akabainisha kuwa katika miaka yote zaidi ya sabini aliyoishi, mnyama huyo akijitokeza, kabila la Wamasai walikuwa wakimjengea kibanda chenye milango minne upande mmoja wakiweka watoto kwa imani kuwa watoto ni baraka, ng'ombe, mbuzi, kondoo na kila wanachoamini ni cha manufaa, na eneo anakopita huamini mafanikio yatatokea kwenye eneo hilo kwani ni kitu ambacho sio cha kawaida kwa kila mtu kuona.

Mkurugenzi wa Kituo cha matengenezo ya Umeme bila kuzima, Live Line, Donald Mwakamele, alisema kupatikana kwa mnyama huyo kituoni hapo, hasa wakati huu ambao serikali imeelekeza nguvu zake kuhakikisha inaongeza uwezo wa nchi kuwa na umeme wa uhakika, inaonyesha umeme utakaozalishwa hautapotea na utawafikia watumiaji inavyopaswa kwavile matengenezo yatafanywa bila kuzima.

# Ukusanyaji maduhuli mtego kwa watendaji idara za ardhi

**Na Munir Shemweta,** MWANZA

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amewaambia watumishi wa Sekta ya Ardhi katika Mkoa wa Mwanza kuwa, wizara itaanza kuwapima wakuu wa idara za ardhi kwenye halmashauri kwa kuangalia utekelezaji wa majukumu yao ikiwamo ukusanyaji maduhuli ya serikali kupitia kodi ya pango la ardhi.

Dk. Mabula alitoa kauli hiyo jana jijini Mwanza wakati akizungumza na wataalamu wa sekta ya ardhi katika mkoa huo akiwa katika ziara ya siku moja kukagua utendaji kazi na kuhamasisha ukusanyaji maduhuli ya serikali kupitia kodi ya pango la ardhi.

Alisema kwa sasa wizara inataka kuona ushindani katika ukusanyaji kodi ya pango la ardhi na wakuu wa idara wanalo jukumu kubwa la kuhakikisha fedha ya kodi ya ardhi inapatikana kwa watendaji hao kuzingatia sheria wakati wa kutekeleza majukumu yao.

"Ninaagiza watendaji wa Sekta ya Ardhi mkasimamie sheria hususan katika ukusanyaji kodi ya ardhi, ninataka ushindani katika makusanyo ya kodi ya pango la ardhi na msimuonee mtu wakati wa utekelezaji majukumu yenu," aliagiza.

Aliwakumbusha watendaji wa sekta kuhakikisha wanafikia malengo ya makusanyo ya kodi ya ardhi kwa kufuata sheria ikiwamo kuwafikisha kwenye Mabaraza ya Ardhi ya Nyumba na Wilaya wadaiwa sugu.

"Mkoa wa Mwanza hamjafanya vizuri katika makusanyo ya kodi ya ardhi, bado mko nyuma sana, asilimia 28 ya malengo na tunafikia nusu mwaka sasa, ni ndogo sana na ni aibu kwa mkoa wakati mnadai takriban Sh. bilioni 70 nje," alionya.

Katika hatua nyingine, Mkoa wa Mwanza katika kipindi cha kuanzia Julai mwaka jana hadi Januari 22 mwaka huu, umefanikiwa kutoa jumla ya hati za ardhi 7,022.

Dk. Mabula alisema wilaya inayoongoza kwa utoaji hati katika mkoa huo ni Ilemela iliyotoa hati 3,212 ikifuatwa na Jiji la Mwanza 2,441, Magu 458, Misungwi 336, Sengerema 216 na Ukerewe 203 huku Wilaya ya Buchosa ikitoa hati 52.

Kwa mujibu wa Dk. Mabula, takwimu katika Mkoa wa Mwanza zinaonyesha kuongezeka kwa kasi ya utoaji hati katika mkoa huo.

Hata hivyo, alisema pamoja na kuongezeka kwa kasi ya utoaji hati, bado mwitikio wa uchukuaji hati kwa wamiliki umekuwa mdogo kulinganisha na uandaaji hati, akidokeza kuwa wamiliki waliojitokeza kuchukua hati wakati wa zoezi la utoaji hati ni 22 huku idadi ya hati zilizoandaliwa ikiwa ni 142.

Aliwataka wamiliki wa ardhi ambao hati zao zimekamilika, kujitokeza kuzichukua na kuongeza kuwa, sasa wamiliki wamerahisishiwa utaratibu wa kupatiwa hati ambapo badala ya kuzifuata ofisi ya Msajili wa Hati Msaidizi Mkoa, wanapelekewa katika halmashauri zao.

Kaimu Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Mwanza, Eliah Kamyanda, alisema ofisi yake imeanza kutekeleza suala hilo kwa kupanga siku maalum za kupeleka hati katika halmashauri husika.

Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Dk. Phillis Nyimbi, aliishukuru Wizara ya Ardhi kwa kujipanga katika kuhakikisha huduma katika sekta ya ardhi zinatolewa kwa ufanisi na kubainisha kuwa sasa katika wilaya yake kuna mwitikio chanya wa wananchi kutaka kumilikishwa ardhi kulinganisha na miaka ya nyuma.

"Wananchi wanapomilikishwa ardhi, hata suala la ulipaji kodi ya pango la ardhi litafanyika kwa ufanisi kwa kuwa kumbukumbu za wamiliki zinafahamika," alisema Dk. Nyimbi.



Diwani wa Kata ya Musanja, Musoma Vijijini, mkoani Mara, Ernest Mwira (kulia) na Mkuu wa Shule ya Sekondari Mabuimerafuru, Jonathan Lucas, wakikagua moja ya jengo la madarasa linalojengwa kwa nguvu za wananchi, shuleni hapo juzi, kwa ajili ya wanafunzi wa kidato cha kwanza. **PICHA: MPIGAPICHA WETU** .

# Rais Mwinyi ateta na Jenerali Mabeyo, Askofu wa Anglikana

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amelipongeza Jeshi la Ulinzi la Wananchi Tanzania (JWTZ) kwa kuendelea na kazi kubwa ya kuimarisha amani na kuilinda mipaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Rais Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana alipokutana na kufanya mazungumzo na Mkuu wa Jeshi hilo, Jenerali Venance Mabeyo, aliyefika Ikulu Zanzibar kwa ajili ya kumpongeza.

Rais Dk. Mwinyi alisema kuwa JWTZ limeendelea kufanya kazi kubwa ya kulinda amani nchini, na kutoa pongezi maalum kwa kuisimamia amani hiyo hasa katika kipindi cha uchaguzi mkuu uliopita.

Alisema wananchi wa Tanzania wanajivunia hatua hiyo ya jeshi lao katika kuhakikisha wanakuwa salama na mali zao wakati wote na kumhakikishia Jenerali Mabeyo kwamba Zanzibar iko salama.

Rais Dk. Mwinyi alieleza kwamba kuwapo kwa ulinzi na usalama kumewafanya wananchi wa Zanzibar kuendelea kufanya shughuli zao za kujiletea maendeleo kwa amani. Alisisitiza kwamba Zanzibar iko salama na kwa vile JWTZ lipo imara, hatua hiyo imewezesha kuimarika zaidi.

"Tumeridhika kwa amani na utulivu uliopo, na tunatoa shukurani kwa kazi nzuri inayofanywa na Jeshi la Ulinzi la Wananchi Tanzania, kwa kulinda mipaka yetu na kuendelea kusimamia amani na utulivu nchini," alisema Dk. Mwinyi.

Aidha, Dk. Mwinyi alieleza haja kwa JWTZ kupitia Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kushirikiana na vikosi vya ulinzi vya Zanzibar kikiwamo kikosi cha Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU), katika suala la uzalishaji mali kama vile kilimo.

Alisema kwa kuwa shughuli zao zinakwenda sambamba kuwapo kwa ushirikiano kutasaidia kwa kiasi kikubwa kuongeza uzalishaji mali katika sekta ya kilimo Zanzibar, hasa ikizingatiwa kwamba JKT ina uzoefu mkubwa katika shughuli hizo.

Kwa upande wake, Jenerali Mabeyo alimpongeza Dk. Mwinyi kwa kushinda nafasi ya urais wa Zanzibar na kueleza imani ya jeshi hilo kutokana na utendaji wake wa kazi.

Alieleza kuwa kutokana na kumfahamu na kuutambua utendaji wa kazi wa Rais Dk. Mwinyi kwa vile aliwahi kufanya kazi naye, ana matumaini makubwa ya kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar. Aidha, Jenerali Mabeyo alipongeza hatua na busara kubwa zilizotumika katika kuleta maridhiano, hali ambayo itazidisha maelewano sambamba na kudumisha amani na umoja nchini.

Pia aliwapongeza wananchi wa Zanzibar kwa kuendeleza amani, umoja na mshikamano na kuahidi kuwa JWTZ itaendelea kutoa ushirikiano kuhakikisha amani inadumishwa katika maeneo yote nchini.

Wakati huo huo, Rais Dk. Mwinyi alikutana na Askofu Michael Henry Hafidh wa Kanisa la Aglikana Dayosisi ya Zanzibar, na kumpongeza askofu huyo pamoja na waumini wote kwa kuendelea kuiombea nchi amani.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mahakama zikatae rushwa kwa vitendo

**JUMAPILI** wakati wa maadhimisho ya Wiki ya Sheria na miaka 100 ya Mahakama Kuu, Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, alikitaka chombo hicho kuhakikisha kinatoa haki kwa wastahili kwa kuzingatia mfumo wa sheria.

Aidha, aliwataka majaji, mahakimu na watendaji wengine wa muhimili huo muhimu katika kutafsiri sheria na kutoa haki kuhakikisha wanatoa maamuzi bila vishawishi vya rushwa.

Kadhalika, alisisitiza kuharakisha matumizi ya lugha ya Kiswahili katika ngazi zote za Mahakama, ili kuwasaidia wananchi wanyonge kupata haki zao za misingi pasipo kikwazo cha lugha.

Alisisitiza umuhimu wa kutoa haki kwa wanaostahili badala ya kutoa haki kwa wasiostahili kwa kigezo cha rushwa na kutambua kuwa haki ni msingi mkuu katika kuimarisha ustawi wa jamii na kama itakiukwa itasababisha migogoro pamoja na kutoweka kwa amani.

Haki ni muhimu katika eneo lolote, ni muhimu zaidi katika mhimili wa kutafsiri sheria kwa kuwa ndipo haki hutendaka kwamba kuna atakayehukumiwa miaka 30 au maisha jela kutokana na uamuzi utakaofanywa na hakimu au jaji.

Hukumu yoyote ile inabadili historia ya maisha ya mtu yeyote kwani kama alikuwa aendelee kuwapo uraiani sasa anakwenda kuishi kifungoni na kila kitu chake kinasimama, ikiwa itakuwa hivyo kwa kuwa ndiyo haki yake kulingana na kosa alilotenda ni sawa kabisa, lakini kama itakuwa hivyo kutokana na shinikizo la rushwa itakuwa ni uonevu mkubwa.

Mara kadhaa kumekuwa na malalamiko dhidi ya baadhi ya wanaotafsiri sheria kuwa rushwa ilitumika kupindisha haki ya fulani na kuambulia hukumu isiyostahili na matukio hayo ni maumivu kwa familia na kizazi chote.

Ni muhimu sana kwa mhimili huo kuwa pamoja na mambo mengine, lakini suala la rushwa na mipango ya kuzuia mianya yoyote ya rushwa likaangaliwa kwa jicho la pekee, ili kuhakikisha haki inatenda vyema kuhakikisha tunakuwa na jamii yenye amani.

Tunatambua kuwa Mahakama imejitahidi kuweka wazi shughuli mbalimbali za uendeshaji kamagharama za kupata nakala ya hukumu, mambo gani ya kulipia na ambayo siyo ya kulipia, kutoa taarifa za hairisho la kesi na mabadiliko mengine ambayo awali hayakuwepo.


Haya yote yanabadilisha utendaji wa kimazoea kiasi cha wananchi kuogopa Mahakama, huku kukiwa na lugha zisizo za kuridhisha hata kwa jambo dogo ambalo mwananchi anataka ufafanuzi, woga ambao wakati mwingine ulitengenezwa ili kutoa mwanya wa rushwa ambayo imewaumiza wengi.

Wananchi wanyonge wanazikimbilia mahakama ili kupata haki iliyoporwa na mtu mwenye uwezo wa kifedha au mamlaka, wanapofika mahakamani na kuumizwa na rushwa ambayo inatumika kama mafuta ya kulainisha maamuzi mbalimbali, wanazidi kuumia kwa kuwa sasa haki yao inapotea si kwa sababu hawakustahili kuipata ila kwa sababu anayepaswa kuitoa ameamua iwe hivyo.

Rushwa ni adui wa haki, ni lazima Mahakama ijiepushe nayo ili ile maana ya kutoa haki itimie na kila mmoja aone haki imetendeka pasipo msukumo wowote.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Yasmine Protace, MKURANGA

# Wauguzi na wakunga, mkasa huu una maana mwenzio akinyolewa...

**KAZI** ni wito na iko kama zingine. Hivyo, inatakiwa mtu aipende kazi yake kwa sababu ndio mtaji wa maendeleo yake.

Tunafanya kazi, lakini tunatofautiana aina ya kazi hizo. Hiyo haijalishi kila mfanyakazi yeyote kupitia kazi yake, anaweza kubadilisha maisha na kupiga hatua yoyote ya kimaendeleo.

Inatakiwa mtu uipande kazi inayokufanya wewe upate ugali na familia yako. Hapo, unaposema kuipenda kazi, tunamaanisha hata wanaokuzunguka katika kazi unayoifanya inatakiwa nao uwapende.

Kama mtu unaipenda kazi yako unapaswa nao kuwapenda wenzako na kama tunashindwa kuwapenda wenzako, basi hautaweza kufanya kazi vizuri.

Pia si busara kuchukua hatua yenye sura ya vipigo kwa vibao mama mjamzito ni kosa kisheria.

Hivi karibuni kumetokea tukio la mtumishi wa kituo cha afya alimpiga mama mjamzito aliyefika kupata huduma nyeti katika kituo hicho.

Ni hali iliyozaa makuu, mhusika kachukuliwa hatua za kisheria.

Nimependa namna Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania, limechukua hatua mara moja katika

Kituo cha Afya Mazwi, muuguzi alilalamikiwa kwa kosa la kumpiga mhitaji wa huduma ya kujifungua kituoni, mwezi huu.

Mwenyekiti wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania, Abner Mathube, alisema Baraza limemtia hatiani mlalalamikiwa chini ya Sheria ya Uuguzi na Ukunga.

Mathube anasema, Baraza lilichambua maelezo ya mlalamikiwa, mlalamikaji pamoja na mashahidi kuhusu kosa la kwanza la kumpiga mgonjwa, jambo ambalo dhahiri ni kinyume na Sheria ya Uuguzi na Ukunga Tanzania.

Katika kosa la kwanza lililotolewa ushahidi, ulithibitisha kuwa mlalamikiwa alimpiga mlalamikaji na mtuhumiwa alikiri kumpiga mlalamikaji.

**Kwa kuzingatia utetezi wa mlalamikiwa na ushahidi uliotolewa na mlalamikaji na mashahidi, umethibitisha mashtaka yote kama alivyoshtakiwa na mlalamikaji," anasema Mwenyekiti wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania na anaendelea: "Muuguzi huyo alipaswa kumuhudumia kwa kwa weledi na upendo mkubwa.**

Ni aina ya madai yalimfikisha mlalamikiwa katika kosa la kushindwa kusimamia maadili na weledi wa kitaaluma. Ilithibitika kuwa mtuhumiwa alishindwa kufuata utaratibu wa utoaji huduma za uuguzi na ukunga kwa mlalamikaji.

Pia ni madai yaliyoenda mbali kwa kushindwa kuchukua na kuhifadhi taarifa za vipimo vya mgonjwa, kushindwa kufuatilia mwenendo wa uchungu wa mgonjwa wakati wa kumpokea katika kituo cha kutoa huduma na kuruhusu mtu ambaye sio mtaaluma kumpima mlalamikaji (mgonjwa).

"Kwa kuzingatia utetezi wa mlalamikiwa na ushahidi uliotolewa na mlalamikaji na mashahidi, umethibitisha mashtaka yote kama alivyoshtakiwa na mlalamikaji," anasema Mwenyekiti wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania na anaendelea: "Muuguzi huyo alipaswa kumuhudumia kwa kwa weledi na upendo mkubwa."

Mwenyekiti katika ufafanuzi wake, kwamba mhusika ameadhibiwa kwa kuondolewa kwenye orodha ya wauguzi na wakunga nchini, kwa mujibu wa sheria zilizopo na ametakiwa kurejesha vyeti na leseni za uuguzi kwa Mkuu wa Mkoa wa Rukwa anayetakiwa, kuziwasilisha kwa Baraza.

Nadhani hapo kuna mawili ninayotathmini, kwamba bado kuna upande mmoja ni kiashiria kuna 'makandokando' ndani ya huduma ya uuguzi yenye mafanikio makubwa sasa na upande wa pili, ni onyo kwa wenye tabia ukiona mwenzio ananyolewa, wewe tia maji'.

# Majaliwa aongoza mazishi ya mbunge

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameshiriki mazishi ya aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum (CCM) Mkoa wa Manyara, Martha Umbulla, na ametumia fursa hiyo kuwasihi wananchi wamuezi kwa kuyaendeleza mambo mema aliyofanya katika kipindi cha uhai wake.

Mazishi hayo yalifanyika jana nyumbani kwake katika kijiji cha Dongobesh wilayani Mbulu mkoani Manyara. Mbunge huyo alifariki Jumanne Januari 21, 2021 katika Hospitali ya HCG Mumbai, India alikokuwa anatibiwa.

"Nimekuja kuungana nanyi kwa niaba ya Mheshimiwa Rais Dk. John Magufuli na Makamu wa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan, kutoa pole kwa mume wa marehemu, watoto na familia kufuatia msiba mzito wa kuondokewa na mpendwa wetu Mheshimiwa Umbulla," alisema.

Waziri Mkuu alisema tukio hilo ni zito na ni ngumu kuishi nalo kwa sababu Martha aliishi vizuri na wabunge wenzake na pia katika kipindi chote cha ubunge wake, aliishauri vizuri serikali.

"Kifo chake ni pigo kubwa kwa serikali, hivyo itaendelea kuthamini na kuuenzi mchango mkubwa alioutoa," Majaliwa alisema.

Alisema jambo la muhimu kwa sasa ni kuendelea kumwomba Mungu ailaze roho ya marehemu mahala pema.

"Mume wa marehemu, watoto, ndugu, jamaa, wabunge na wananchi wa Mkoa wa Manyara ninamwomba Mwenyezi Mungu awape moyo wa uvumilivu na subira katika kipindi hiki kigumu," alisema.

Naibu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, akizungumza kwa niaba ya Spika wa Bunge, Job Ndugai, alisema Bunge limempoteza mtu muhimu na litamkumbuka Martha kwa mchango mkubwa alioutoa enzi za uhai wake.

Alisema Martha alikuwa mlezi kwa wabunge wapya wanaoingia bungeni.

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul, akizungumza kwa niaba ya wabunge wa Mkoa wa Manyara, alisema Martha aliwafundisha mambo mengi ikiwamo kufanya kazi kwa bidii, upendo, uvumilivu, kusamehe na kuomba msamaha pamoja na kumcha Mwenyezi Mungu.

"Dada Martha hakuwa mbunge wa kawaida," Gekul alisema, alipomwelezea mbunge mwenzake huyo.

Awali, akisoma wasifu wa marehemu, mtoto wa kwanza wa Martha, Innocent Umbulla, alisema mama yao alizaliwa Novemba 10, 1955 katika Kijiji cha Dongobesh wilayani Mbulu na alikuwa mtoto wa mwisho katika familia ya watoto wanne.

Alisema mwaka 1963 hadi 1969, alipata elimu ya msingi katika Shule ya Msingi Dongobesh na baadaye aliendelea na masomo ya sekondari katika Shule ya Wasichana ya Korogwe mwaka 1970 hadi 1973. Mwaka 1974 hadi 1975, alisoma Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Tabora. "Mwaka 1976, alihudhuria kwa mujibu wa sheria mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) Kambi ya Ruvu na mwaka 1977 hadi 1979 alisoma stashahada ya kilimo katika Taasisi ya Kilimo Ukiliguru Mwanza.

"Mwaka 1989 hadi 1990, alisoma shahada ya juu katika Chuo cha Reading, Uingereza na mwaka 2000 hadi 2002, alisoma shahada ya uzamili katika fani ya usimamizi wa biashara Uholanzi," alisema.

Alisema mama yao alifanyakazi katika maeneo mbalimbali ikiwa pamoja na ukufunzi katika Taasisi ya Kilimo Ukiliguru, Mkufunzi Mbobezi wa Maofisa Ugani katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mkuu wa Wilaya ya Kongwa na Kiteto.



Ofisa wa Benki ya KCB Tanzania, tawi la Arusha, Tumaini Swai (kushoto), akikabidhi zawadi ya vifaa vyenye thamani ya Sh. laki 5 kwa mshindi wa shindano la programu ya ujasiriamali ya 2jiajiri, Theodora Tarimo (katikati), katika hafla iliyofanyika tawini hapo, jana. Kulia ni Ofisa Biashara wa benki hiyo, Renatus Mroso. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mipaka yakumbukwa huduma za mawasiliano

**Na Mwandishi Wetu**

MTENDAJI Mkuu wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF), Justina Mashiba, amesema mfuko huo umeanza kutekeleza miradi ya kupeleka huduma za mawasiliano katika maeneo ya mipakani kwa lengo la kuhakikisha wananchi wa maeneo hayo wanapata huduma.

Mashiba amesema lengo lingine la uhakiki huo ni kuhakikisha usalama wa nchi.

Aliyasema hayo wakati wa halfa ya utiaji saini mikataba mitatu iliyosainiwa kati ya UCSAF na kampuni za simu za Vodacom, Artel na Tigo ambazo zinapeleka huduma za mawasiliano katika vijiji 173 vilivyo katika kata 61.

Kampuni ya Airtel Tanzania inapeleka mawasiliano katika vijiji 73 kutoka katika kata 25 kwa ruzuku ya shilingi bilioni 2.7, kampuni ya Vodacom inapeleka mawasiliano katika vijiji 63 kwa ruzuku ya shilingi bilioni 2.6 na kampuni ya Tigo itapeleka mawasiliano katika vijiji 31 katika kata 13 kwa ruzuku ya Sh. bilioni 1.5

Tukio la utiaji saini lilishuhudiwa na Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Faustine Ndugulile, aliyeambatana na Naibu Waziri, Mhandisi Andrea Kundo, Katibu Mkuu, Dk. Zainab Chaula, Naibu Katibu Mkuu Dk. Jim Yohazi na baadhi ya watendaji wa wizara hiyo.

Dk. Ndugulile aliipongeza UCSAF na kuongeza kuwa utiaji saini huo ni kielelezo cha ushirikiano mzuri kati ya serikali na kampuni binafsi, na kusema kuwa hatua hiyo ni ya kupongezwa. Aidha, aliitaka UCSAF kwa kushirikiana na kampuni za simu kuongeza wigo wa upelekaji huduma za mawasiliano.

Wakati huo huo, Dk. Ndugulile ametoa onyo kwa kampuni za simu ambazo baadhi ya watumishi wake wamekuwa wakitoa taarifa za wateja bila kufuata utaratibu huku akiitaka Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kufuatilia na kampuni itakayobainika itachukuliwa hatua za kisheria.

Naye Naibu Waziri, Mhandisi Andrea Kundo, alisema mahitaji ya mawasiliano yanazidi kuongezeka na ili kukidhi mahitaji hayo, kunahitajika uwekezaji katika kufanya utafiti na uvumbuzi wa teknolojia ambayo inaweza kutumika vizuri nchini kwani mawasiliano yanaenda kuwa moja ya njia kuu za kukuza uchumi.

Kwa upande wake Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Zainab Chaula, alisisitiza kukamilika kwa wakati kwa miradi hiyo na kuwataka wadau hao kutimiza kuzingatia makubaliano yaliyofikiwa.

# DC apokea ripoti shida ya tope

**Na Christina Mwagala**

MKUU wa Wilaya ya Kinondoni, Daniel Chongolo, amepokea ripoti ya utafiti iliyofanywa na wataalamu wa jiolojia kuhusiana na kuwapo kwa tatizo la tope katika eneo la Kunduchi jijini Dar es Salaam Novemba mwaka jana.

Chongolo alipokea taarifa hiyo jana ofisini kwake kutoka kwa timu ya wataalamu iliyokuwa inachunguza tatizo hilo ikiongozwa na Mhadhiri wa Jiolojia kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dk. Remigius Gamba.

Akizungumza baada ya kupokea ripoti hiyo, Chongolo alisema serikali ilichukua hatua ya kuunda kamati ya wataalamu kwa ajili ya kuchunguza hali hiyo na hivyo kuipongeza kutokana na kazi kubwa waliyoifanya.

Chongolo aliwataja wataalamu waliohusika katika utafiti wa suala hilo kuwa ni kutoka Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (AGST), UDSM kupitia Shule ya Migodi na Madini Idara ya Jiosayansi, Baraza la Taifa la Mazingira (NEMC) na Chuo cha Mafunzo ya Jiosayansi (AMGC).

Aliongeza kuwa kupitia ripoti hiyo, ushauri uliotolewa na wataalamu hao, utafanyiwa kazi kwa pamoja kama serikali kuanzia ngazi ya wilaya hadi ngazi za juu zinazohusiana na uchakataji wa taarifa pamoja na utekelezaji wake.

Chongolo alisema utafiti huo ulikuwa ukifanyika kwa kushirkiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Abubakari Kunenge na kwamba kutokana na umuhimu huo, ataiwasilisha kwake ili ajue matokeo ya uchunguzi wa kamati hiyo.

K COM
TUNA AJIRI
SALES EXECUTIVE
VIGEZO VYA KAZI:
- Cheti cha Form IV
- Muajiriwa awe anaweza kuongea na kuandika Kiingereza na Kiswahili.
WASILIANA KWA 0624279186
Email: deotrophis@gmail.com

# JPM kuzuru Shinyanga kesho

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Zainabu Telack, amesema kuwa kesho kutakuwa na ziara ya Rais John Magufuli mkoani humo, kiongozi huyo wa nchi akitarajiwa kutembelea viwanda na kuweka jiwe la msingi katika jengo la wagonjwa wa nje kwenye Hospitali ya Wilaya ya Kahama.

Telack aliyasema hayo jana mjini Kahama alipozungumza na waandishi wa habari na kubainisha kuwa Rais atakuwa na ziara ya siku mbili yenye lengo la kuangalia utekelezaji wa ilani ya chama.

Alisema kuwa katika ziara hiyo, Rais Magufuli ataweka jiwe la msingi katika kiwanda cha Kahama Food Product LTD kinachomilikiwa na mwekezaji mzawa Mhoja Nkwabi kinachozalisha maji, juisi na soda.

Mkuu wa mkoa huyo alisema Rais Magufuli atakagua jengo la wagonjwa katika Hospitali ya Wilaya ya Kahama iliyojengwa kwa Sh. bilioni 3.9 na mradi wa maji uliopo Kijiji cha Isaghehe, Kagongwa na Isaka na unaowanufaisha wananchi zaidi ya 50,000 uliogharimu Sh. bilioni 24.

Alisema wameamua kujenga jengo la utawala na wagonjwa wa nje kwa kuwa kulikuwa na tatizo la msongamano wa wagonjwa hasa wanawake wanaokwenda kujifungua, akibainisha kuwa kwa siku watoto 35 hadi 75 wanazaliwa.

"Kijiji cha Chapulwa tumetenga eneo la ukubwa wa ekari 60 ambapo eneo hilo kuna viwanda vya aina mbalimbali kama kiwanda cha maziwa, kiwanda cha nafaka na chakula cha mifugo pamoja na kiwanda cha magodoro na wawekezaji wamekwishajitokeza," alisema Telack.

Alisema kuwapo kwa eneo la uwekezaji huku wanawake wakipewa kipaumbele kupata maeneo kwa ajili ya kuendesha shughuli zao, kunatarajiwa kutoa ajira kwa watu 2,000.

Telack alisema wametoa eneo hilo la uwekezaji kwa muda wa miezi sita kama mtu akishindwa kuliendeleza, atanyang'anywa.

# Njombe walia uhaba wa dawa

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

CHANGAMOTO ya uhaba wa dawa katika vituo vya huduma za afya wilayani Ludewa mkoani Njombe imezua malalamiko miongoni mwa wananchi.

Baadhi yao wamelalamikia fedha zao za michango yao ya Mfuko wa Bima ya Afya ya Jamii (CHF) iliyoboreshwa.

Katika mkutano wa hadhara wa Mbunge wa Ludewa, Joseph Kamonga, akiwa katika mwendelezo wa ziara yake jimboni humo, Diwani wa Ludewa Mjini, Monica Mchiro, alisema changamoto ya uhaba wa dawa imekuwa ikimpa wakati mgumu kutokana na wananchi wake kumhoji mara kwa mara.

"Kwa kweli wananchi wanalalamika sana, watu wanaolipa CHF na wasiolipa wote wanaambiwa wakanunue dawa...mimi nilivyoliona hilo nilifika hospitali na viongozi wa kata tuliambiwa kuna vyanzo vitatu vya CHF na mfuko wa Basket Fund pia ruzuku kutoka Serikali Kuu," alisema Mchiro.

Baada ya kupokea changamoto hiyo, Mbunge Kamonga aliamua kutembelea Hospitali ya Wilaya ya Ludewa ili kuona uhalisia wa malalamiko hayo ambapo uongozi wa hospitali hiyo chini ya Mganga Mkuu wa Wilaya, Dk. Stanley Mlay, ulikiri kuwapo kwa changamoto hiyo miezi ya nyuma na kuwa tatizo lilisababishwa na ugonjwa wa corona.

"Kulikuwa na upungufu wa dawa kipindi cha nyuma, lakini tumejitahidi kulitatua kadri ya uwezo kulingana na hali tulionayo, dawa za msingi zote zipo na ambazo zimepungua tumejitahidi kuagiza MSD na kuendelea kuongeza makusanyo ili kuona changamoto ya dawa haijitokezi tena," alisema Dk. Mlay.

Mmoja wa wagonjwa wanaopata matibabu katika hospitali hiyo, Elnest Kowi, alisema wamekuwa wakihudumiwa vizuri, huku akiomba huduma kuendelea kuboreshwa zaidi.

Mbunge baada ya kutembelea na kukagua hospitali hiyo, alieleza kujiridhisha na uwapo wa dawa za kutosha, huku akiwataka wananchi kuendelea kwenda kupata huduma.




Meneja Idara ya Kadi wa Benki ya NMB, Sophia Mwamwitwa (katikati), akikabidhi jokofu jipya kwa Rose Marealle mkazi wa Mbezi Inn, baada ya kuibuka mshindi kwenye shindano la MastaBATA, jijini Dar es Salaam jana. Mteja huyo amejishindia jokofu, 'cooker', mashine ya maji na mashine ya kupashia chakula baada ya kutumia card ya NMB Mastercard kufanya miamala na manunuzi mbalimbali. Kushoto ni Meneja wa Benki ya NMB Tawi la Mbezi Louis, Nestory Mwombeki.. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wasichana waandaliwa mapinduzi ya viwanda

**Na Beatrice Shayo**

WASICHANA 20 wanaosoma katika Shule ya Sekondari ya Temeke jijini Dar es Salaam ambao wamepewa mafunzo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), wametakiwa kuitumia elimu hiyo iwasaidie katika mapinduzi ya nne ya viwanda.

Akizungumza wakati wa mahafali iliyofanyika katika shule hiyo, Meneja Mradi wa Shirika lisilo la kiserikali la BRAC Maendeleo, Veronica Kamwela, alisema limejitolea kutoa fursa hasa kwa wanawake na wasichana ili waweze kufikia malengo yao kiuchumi.

Alisema BRAC wamekamilisha mafunzo yao rasmi kwa wanafunzi hao ambao walishiriki katika kipindi cha mwaka mmoja kupitia mradi unaoitwa 'Skill for their Future" unaodhaminiwa na shirika la kimataifa la TheirWorld.

Alisema kupitia mradi huo wanafunzi hao wa kidato cha tatu wanaochukua mchepuo wa masomo ya Sayansi walipata mafunzo mbalimbali ya TEHAMA, kuandika code na ujasiriamali ili kuwaandaa katika mapinduzi ya nne ya viwanda.

"BRAC, tunatekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ambayo inalenga kuwawezesha wasichana na wanawake kijamii na kiuchumi. Tuna furaha kubwa kukamilisha mradi huu kwa mafanikio makubwa. Lengo kuu la mradi huu lilikuwa ni kuwawezesha wasichana hawa 20 kwa kuwapatia ujuzi wa TEHAMA, lakini walimu pia wamenufaika kupata mafunzo ya kutumia kompyuta," alisema.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Ingia Mtenga, aliishukuru BRAC kwa kuchagua shule yao kwa ajili ya kutekeleza mradi huu na kuwajengea uwezo wanafunzi hao.

"Kupitia mradi huu shule yetu imepata maabara na kompyuta ambazo zitaendelea kuwa mali ya shule, hivyo kuendelea kunufaisha wanafunzi zaidi," alisema.

Aidha, alisema walimu wao 18 wamepata fursa ya kupata ujuzi wa msingi wa TEHAMA kama sehemu ya mradi huo mwaka 2020.

Wakati huo huo, BRAC Maendeleo pia ilichangia taulo za wasichana 750 wanaoshiriki katika miradi miwili ya uwezeshaji vijana inayoitwa Goal na ELA kupitia klabu za vijana rika.

# RC Mtaka alipa angalizo Jeshi la Polisi

**Na Happy Severine,** BARIADI

MKUU wa Mkoa wa Simiyu, Anthony Mtaka, amevitaka vyombo vinavyohusika na ukamataji wa watuhumiwa na kupeleleza kutenda haki pamoja na kutanguliza utu.

Alisema wakati mwingine haki inakosekana kwa watuhumiwa kutokana na vyombo ambavyo vinahusika katika ukamataji na upelelezi kutotekeleza majukumu yao kwa haki pamoja na kutokuwa na utu.

Alisema hayo jana wakati wa uzinduzi wa Wiki ya Sheria na maadhimisho ya miaka 100 ya mahakama mjini Bariadi.

Mtaka alilitaka Jeshi la Polisi kubadilika katika utendaji kazi wake, kwani haki ya mtuhumiwa huanza kupotea kwenye eneo lao kabla ya kufikishwa mahakamani, hali ambayo watu wengi wamefungwa bila ya hatia.

Alisema malalamiko ya watu kusingiziwa na kubambikizwa kesi mbalimbali yamekuwa mengi na Jeshi la Polisi limekuwa likilalamikiwa kwa tabia hiyo na kuwataka kubadilika ili haki iweze kutendeka.

"Ikiwa mkamataji na mpelelezi wakisema uongo, hapo hakuna haki hata kidogo, wala hakimu au mahakama inaweza kushindwa kupata ukweli ikaonekana uongo wa polisi ndiyo ukweli na mtu akapewa adhabu kumbe siyo kweli.

"Misingi ya haki na utu ianzie kwenye Jeshi la Polisi, hawa ndiyo wahusika wa awali kabisa kwenye kesi yeyote, kama hivyo vitu havitakuwapo ni ngumu mtu mnyonge kupata haki, ni vyema polisi mkabadilika kwenye hilo," alisema Mtaka.

Awali akizungumza kwenye uzinduzi huo, Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Shinyanga, Gerson Mdemu, alisema katika wiki hiyo watu watapata fursa ya kupewa elimu ya jinsi mahakama inavyofanya kazi kwa haki.

Jaji Mdemu aliongeza kuwa wamepanga kutumia wiki hiyo kuwafikia watu wote kwenye maeneo ya minada na magulio lengo likiwa kila Mtanzania kupewa elimu ya sheria pamoja na kutambua utendaji kazi wa muhimili huo wa nchi.

"Wananchi mnatakiwa kujitokeza kwa wingi kupitia maadhimisho haya, kwa wiki nzima tutakuwa hapa Bariadi, tutakwenda kwenye minada na magulio, hivyo tunaomba mjitokeze kwa wingi mkapate elimu hii," alisema Jaji Mdemu.

# Wakulima, wafugaji wavamizi wa maeneo waamriwa kuondoka

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amewataka wafugaji na wakulima wanaoendesha shughuli zao katika maeneo ambayo hayajaruhusiwa kuondoka mara moja.

Amewataka kuendesha shughuli zao katika maeneo waliyotengewa kisheria, na kwamba watakaokiuka agizo hilo watachukuliwa hatua kali.

Ndaki alisema serikali imetenga maeneo mahsusi kwa ajili ya wakulima na wafugali, hivyo hakuna haja tena ya pande hizo mbili kuanza kuvamia katika maeneo ambayo hawajaruhusiwa na kuwataka kutii sheria.

Ndaki aliwataka wakulima walioingilia katika eneo la malisho ya mifugo katika vijiji vya Amei, Loolera, Lesoit na Lembapuri vilivyopo Kata za Loolera na Lengatei wilayani Kiteto mkoani Manyara na kuanza kufanya shughuli za kilimo, waondoke mara moja katika eneo hilo kwa kuwa wanachangia migogoro.

"Haya mambo ya wakulima na wafugaji kuvamia maeneo ambayo hawajaruhusiwa ndiyo inachangia hii migogoro, na ninaomba iwe mwisho vifo vinavyotokana na migogoro hii," alisema Ndaki.

"Hatutamvumilia yeyote anayesababisha migogoro hii na kusababisha vifo kama ilivyotokea hivi karibuni, huu uwe ndio mwisho."

Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Joseph Mkirikiti, aliwataka wakulima kuacha kulima kwenye ukanda wa malisho katika Wilaya ya hiyo ya Kiteto kwa kuwa hairuhusiwi kufanya hivyo.

"Uongozi wa kijiji ndiyo wenye mamlaka yote kupitia mkutano mkuu, kugawa maeneo kwa ajili ya matumizi mbalimbali yakiwamo ya kilimo na ufugaji," alisema na kuendelea:

"Ninawataka watu wote ambao wamepewa maeneo ya kilimo kinyume cha utaratibu wafike katika ofisi ya mkuu wa wilaya ya Kiteto ili kujua hatima yao, na ninataka waliohusika katika hili hata kama ni viongozi watachukuliwa hatua kali."

Pia alipiga marufuku baadhi ya watu ambao wamekuwa wakifanya shughuli za udalali wa ardhi katika Wilaya ya Kiteto kwa kuwauzia wengine wanaotoka nje ya wilaya hiyo maeneo ya malisho ya mifugo kwa kuwadanganya kuwa ni ya kilimo.



Abiria wakilazimika kumsaidia dereva wa bajaji, kuikwamua kwenye maji baada ya kukwama kwenye mchanga, wakati akitaka kuvuka Mto Tegeta, eneo la Goba Tegeta A, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Baadhi ya walimu wadaiwa kushindwa kusimamia miradi

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

BAADHI ya wakuu wa shule za msingi na sekondari wamedaiwa kushindwa kusimamia vyema miradi ya serikali inayotekelezwa katika maeneo yao na kusababisha kushindwa kukamilika kwa wakati au kutekelezwa chini ya kiwango.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, alisema hayo mjini Morogoro wakati akifungua mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Tume ya Utumishi wa Walimu.

Alisema katika ziara yake maeneo mbalimbali nchini, alibaini kero kubwa iliyopo ni kwa wakuu wa shule hizo za msingi na sekondari kushindwa kusimamia ipasavyo miradi ya serikali katika maeneo yao.

"Kuanzia sasa nawaagiza watumishi wa Tume mkasimamie vizuri miradi hiyo," alisema.

Aliitaka Tume hiyo kuhakikisha walimu wanajitambua na kuelewa sheria, kanuni, taratibu haki na wajibu wao huku serikali ikiendelea kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili na kwamba ushirikiano uliopo katika utendaji kazi kati ya Tume na TAMISEMI ni endelevu.

Aliwataka wakurugenzi wa halmashauri za wilaya kote nchini kuhakikisha wanawapatia makatibu wasaidizi wa Tume ya Utumishi ya Walimu ofisi zenye hadhi za tume tofauti na ilivyo sasa.

Mwenyekiti wa Tume hiyo, Profesa Willy Komba, alisema licha ya tume hiyo kuwa na majukumu ikiwamo kusimamia nidhamu na utendaji wa kazi za walimu, bado wanakabiliwa na kero mbalimbali ikiwamo ya ufinyu wa bajeti unaokwamisha utekelezaji hususani ya kisheria na utoaji elimu kwa walimu.

Alisema kero nyingine ni baadhi ya waajiri kutozingatia sheria, kanuni na taratibu katika kushughulikia masuala ya kinidhamu ya walimu.

"Mfano kumekuwapo na ucheleweshaji wa uwasilishaji wa mashtaka kwa mamlaka ya nidhamu, kuchukua jukumu la kutoa adhabu kinyume cha utaratibu na kuwaondoa walimu kwenye payroll (mfumo wa malipo) kabla ya mchakato wa mashauri kuanza na kukamilika," alisema Profesa Komba.

Pia kwa baadhi ya waajiri kuchelewa kujibu barua za walimu.

# Madereva 1,000 mbaroni madai kukwepa kulipa faini

**Na Christina Haule,** MOROGORO

ZAIDI ya madereva 1,000 wa magari ya aina mbalimbali wamekamatwa mkoani Morogoro, kwa madai ya kudaiwa madeni ya faini za makosa mbalimbali.

Kamanda wa Polisi mkoani hapa, Fortunatus Musilimu, alisema madereva hao waliokamatwa kwenye operesheni iliyoanza kufanywa na polisi tangu Januari 18 hadi jana, ambapo jumla ya madereva 1,384 wameshakamatwa.

Kamanda Musilimu alisema operesheni hiyo ni endelevu ambayo inafanyika nchi nzima kwa magari ya aina zote kutoka mikoa mbalimbali.

Alisema hapo mwanzo madereva walikuwa wanapaswa kulipa madeni papo hapo wanapokamatwa na makosa, lakini kutokana na kuwapo malalamiko kuwa hawatendewi haki wakaruhusiwa kulipa baadaye.

"Malalamiko yao wengine wanakamatwa wakati hawana fedha kwa wakati huo, na wengine wanapokamatwa wanaenda kulipa vituo vya polisi vilivyo mbali huku wakiwa wanapaswa kuendelea na safari," alisema.

Alisema serikali ya sasa ni sikivu ikasikia kilio chao na kuamua kuweka mfumo na utaratibu wa kuwapa siku saba za kuwawezesha kulipa madeni pale wanapokutwa na faini jambo ambalo limeonekana kupuuzwa.

Alisema madereva hao hawalipi faini hizo, hivyo Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani kuendelea kuwatafuta.

Alisisitiza kuwa madereva wote wanaodaiwa faini za makosa ya usalama barabarani walipe na kwamba hawatapita kama hawatalipa.

Pia Musilimu alisema jumla ya pikipiki 396 zimekamatwa kutokana na makosa mbalimbali ya usalama barabarani ikiwamo kutovaa kofia ngumu, kubeba abiria zaidi ya mmoja (mshikaki).

Kamanda huyo alisema kati ya pikipiki hizo zilizokamatwa, 354 zimeandikiwa faini, 22 zilipewa onyo (PF.6) na 20 bado zipo kituoni baada ya madereva wa pikipiki hizo kukimbia wakati wa ukamataji.




Mkuu wa Mauzo na Usambazaji wa Vodacom Tanzania Plc, George Lugata, akizungumza na waandishi wa habari, wakati wa uzinduzi wa simu mpya za kisasa aina ya Tecno RC6 (Tecno Babkubwa) na Itel AC13 (Itel Kitonga), jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Meneja Uhusiano wa Itel, Fernando Wolle. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TAKUKURU yaokoa mil. 58/- miezi mitatu Pwani

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Pwani katika kipindi cha miezi mitatu imeokoa Sh. 58,195,184 katika maeneo mbalimbali.

Naibu Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Pwani, Sadiki Nombo, alisema kuokolewa kwa fedha hizo kumetokana na ushirikiano kutoka kwa wananchi wa maeneo husika na taasisi hiyo, baada ya kufanyika uchunguzi tuhuma zilizowasilishwa.

Nombo alisema katika ofisi ya TAKUKURU Wilaya ya Kibiti, kiasi cha Sh. 18,007,384 ziliokolewa ikiwamo Sh. 8,130,384 kutoka kwa viongozi wa vyama vya ushirika vya msingi (AMCOS) fedha ambazo ziligawiwa kwa wakulima waliokuwa wanadai.

Aidha, alisema kiasi cha Sh. 8,877,000 ziliokolewa kutoka katika vikundi vya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu, ambazo zilikopeshwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti na kushindwa kurejeshwa.

Naibu Mkuu huyo wa TAKUKURU alisema ofisi ya Taasisi hiyo Wilaya ya Kibiti iliokoa pia kiasi cha shilingi milioni moja baada ya Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Msafiri kuzitumia kinyume cha utaratibu.

Akizungumzia Wilaya ya Chalinze, alisema kiasi cha Sh. 3,950 ziliokolewa, ambapo kati ya hizo, shilingi milioni tatu ziliokolewa kwa kushirikiana na Wakala wa Misitu (TFS).

Ndomba alisema TAKUKURU iliingilia kati uvunaji wa magogo ya miti uliofanywa na wafanyabiashara haramu wa misitu waliokuwa wanakata miti aina ya mikaratusi katika maeneo yasiyoruhusiwa.

Sh. 600,000 zilizokuwa zimechepushwa na viongozi wa Kijiji cha Muhoro baada ya kupokea faini kwa wafugaji waliolisha mifugo yao kwenye mashamba ya wakulima ziliokolewa, na Sh. 350,000 zilirejeshwa kwa mkulima wa korosho.

## Washindi NMB MastaBATA waendelea kuzoa mamilioni

**Na Mwandishi Wetu**

WASHINDI 12 wa droo ya nane ya NMB MastaBATA, wamepatikana na kujizolea zawadi zenye thamani ya Sh. milioni 28.8, hivyo kufanya zawadi zilizotolewa kufikia thamani Sh. milioni 87.6 kati ya zaidi ya Sh. milioni 200 zinazoshindaniwa.

NMB MastaBATA inayoendeshwa na Benki ya NMB, ni kampeni inayolenga kuhamasisha matumizi na manunuzi kwa Kadi za NMB Mastercard na Masterpass QR, ilianza Novemba 24, 2020, ikitoa zawadi za Sh. 100,000 kwa washindi 40 kila wiki na washindi 12 wa Sh. milioni 2.4 kila mwezi.

Akizungumza jana wakati wa droo hiyo ambayo ni ya pili kati ya tatu za mwezi, Mkuu wa Biashara ya Kadi wa NMB, Philbert Casmir, amesema katika droo saba zilizotangulia (sita za wiki na mbili za mwezi), zimewawezesha washindi 304 kujizolea zawadi za Sh. milioni 87.6.

Casmir alibainisha kuwa, NMB MastaBATA imebakisha droo 3 kukamilisha miezi mitatu ya kampeni hiyo, ambayo zawadi kuu 'Grand Finale' itakuwa ni ziara ya utalii Zanzibar, Ngorongoro ama Serengeti, iliyolipiwa kila kitu na benki ya NMB, ambako washindi watakuwa huru kuchagua zawadi mbadala.


"Wito wetu kwa wateja wa NMB kuendelea kufanya matumizi na manunuzi mbalimbali kwa Kadi za NMB Mastercard na Masterpass QR, ili kujiongezea nafasi sio tu ya kushinda zawadi za wiki na mwezi, bali ziara hii ya kitalii katika moja kati ya maeneo hayo matatu," amesema Casmir.

Katika droo ya jana, iliyofanyika chini ya usimamizi wa ofisa kutoka Bodi ya Michezo Kubahatisha Tanzania (GBT), Pendo Albert, washindi 12 walikuwa huru kuchagua zawadi zilizogawanywa katika makundi matatu, kila moja likiwa na zawadi zenye thamani ya Sh. milioni 2.4.

## Mbatia: Wapinzani kususa hakutoi majibu, bali 'tukomalie' meza moja



Ukurasa 12



Ukurasa 13

RAIS SAHLE - WORK ZEWDE

## Mwanamama aliyekanyaga Tanzania juzi, amefungasha neema ushirikiano


# siasa

JUMATANO JANUARI 27, 2021

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe




Ukurasa 14

## Huyu ndiye Lucy Lameck

# MWEZI JANUARI; MAMA MAJANGA SIASA AFRIKA

• Miaka 50 Amin kupindua • Miaka 20 kuuawa Kabila • Miaka 10 janga la Mubarak

**Na Ani Jozeni**

SIYO kila kumbukumbu inayoenda na matukio yanayoleta simanzi. Ila kwa hali yoyote ile, yapo yasiyosahaulika, kama vile kupinduliwa serikali ya Rais Dk. Milton Obote nchini Uganda, mnamo Januari 25, 1971.

Ni tukio lililoathiri siasa nchini Tanzania, kwani serikali ya TANU ilipata picha ya hatari iliyoko mbele yake kutokana na njama za serikali kubwa nchi za nje zinazochukia msimamo thabiti wa Tanzania dhidi ya ubaguzi wa rangi na kuunga mkono harakati za ukombozi Kusini mwa Afrika.

Ilikuwa tukio lililolazimisha TANU kuchukua hatua kuwa karibu na wananchi, utamaduni wa siasa nao kubadilika.

Kilicholeta fedhaa nchini, hasa kwa Rais Julius Nyerere, ni kwamba kupinduliwa Dk. Obote haikuwa tu suala la raia wa Uganda na vikosi vya jeshi au makamanda wake akiwamo mkuu wa jeshi Jenerali Amin kutaka kumwondoa madarakani, ila lilipangwa kwa kushirikiana na mataifa ya nje.

Ni mazingira yaliyopata madai, kwamba kiongozi mkuu wa nchi hiyo ya kigeni katika mkutano huo wa Jumuiya ya Madola, aliwabeza baadhi ya viongozi wa nchi za Afrika wakiwa katika mkutano wa Jumuiya ya Madola jijini Kuala Lumpur, Malaysia, akisema baadhi wasingerudi nyumbani.

Alijua fika kuwa kabla ya jua kuchomoza kesho yake, serikali ya Rais Obote, itakuwa imepinduliwa na yeye uhamishoni.



Aliyekuwa Rais Idi Amin Dada. **PICHA: MTANDAO**

**TAFAKARI INAKOANZA**

Ni kuanzia hapo, TANU ilitafakari na matokeo yake yalizaa Mwongozo wa TANU uliopitishwa na ukawa halisi ukisimamia shughuli muhimu za kisiasa na kiuchumi kitaifa.

Sababu ilikuwa kuhakikisha kuwa chama kinahusika kila mahali, ili maadui wasipenyeze kupitia njia za kirasimu, waunde vikundi, wasijitenge na uongozi kutoa mwanya wa njama dhidi yake.

Hivyo nguvu ya chama zikawa siyo tu kushika hatamu bungeni (kupitisha sheria), pia katika ulinzi wa nchi.

**RAIS KABILA**

Kumbukumbu ya kuuawa Rais Laurent Kabila nchini Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), Januari 16, mwaka 2001 ni tukio kubwa lingine.

Ni kuanzia wimbi la vita kuondoa utawala wa Rais Mobutu Seseseko, yeye akiwa mgonjwa ng'ambo (akafia Morocco) ilihaibika kabisa.

Papaa Kabila anadaiwa kuuawa na watu wa karibu yake, kutokana na ugomvi uliozuka kati yake na serikali ya Rwanda, ambayo kwa sehemu kubwa ilimsaidia kuunganisha nguvu ya kuondoa utawala wa Mobutu.

Jeshi la Zaire (ikiitwa hivyo wakati huo) lilikuwa halina itikadi ya pamoja au kiongozi, ila Mobutu awepo hapo.

Kuuawa kwa Papaa Kabila kuliitumbukiza DRC na eneo la katikati ya Afrika vitani na vurugu za kisiasa, nchi za upande wa kusini zikipambana na vikosi vya Rwanda na washirika wao ndani ya DRC.

Mwisho wake, Rwanda na marafiki zake wakarudi nyuma, wakaishia kulinda maslahi yao. Ni hali ambayo kimsingi imedumu na hadi sasa makundi tofauti yanapambana baina yao na zaidi kupigana na jeshi la nchi linalotaka sheria.

**MISRI NAKO**

Ripoti za vyombo vya habari kuhusu aliyekuwa Rais wa Misri, marehemu Hosni Mubarak, alichukua utawala baada ya Rais Anwar Sadat kupigwa risasi na askari aliyekuwa akishiriki gwaride, vuguvugu lenye mzizi mwezi Januari na akafa tarehe 25 ya mwezi uliofuata, Februari.

**INAENDELEA UK.12**

# Mbatia: Wapinzani kususa hakutoi majibu, bali 'tukomalie' meza moja

**Na Sabato Kasika**

SEHEMU ya mambo ambayo Kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD), kinaamini, kwamba yana mchango mkubwa katika kuimarisha vyama vya siasa ni kukaa pamoja na kujadiliana jambo la siasa, ili kujengeana uaminifu na kuepusha migogoro ndani ya vyama vya kisiasa.

Mwenyekiti wa TCD ambaye ni Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha NCCR-Mageuzi, James Mbatia, amekuwa akihimiza hilo katika kauli zake akiamini hiyo njia mojawapo muhimu ya kuimarisha vyama vya siasa.

Wakati akifungua majadiliano ya vyama vya siasa ngazi ya taifa kwa lengo la kutatua migogoro ndani ya vyama, hivi karibuni anasema njia hiyo inajenga uaminifu kwa kuwa na maridhiano ya pamoja na kujenga jamii yenye umoja.

Ni kauli ambazo hata tangu kumalizika uchaguzi mkuu, Mbatia amekuwa akiwahimiza wanasiasa kukaa meza moja ya mzungumzo kumaliza sintofahamu zilizopo kati yao, hali iliyojitokeza pale baadhi ya vyama kutotambua matokeo ya uchaguzi huo. Baada ya uchaguzi huo, kuna vyama vya siasa vilikuwa vikitoa matamshi ya maalamiko yakiwamo ya kukiri kuwa uchaguzi ulikuwa 'huru na haki' na vingine vikidai kwamba uligubikwa na kasoro nyingi.

Kuna vyama vimegoma kutambua matokeo ya uchaguzi huo na kudai kwamba havioni sababu ya kushiriki siasa na vikitamka kujiweka pembeni na siasa zilizoko kitaifa.

### KUKAA PAMOJA

Hata hivyo, Mwenyekiti wa TCD anajipambanua kuwa ameweka mbele zaidi maslahi ya taifa kwa kujali meza ya mazungumzo ya pamoja, ili kuja na muafaka unaohusiana na uchaguzi huo.

Mbatia anawasilisha imani yake kwamba yapo madai ya 'figisufigisu' kwenye uchaguzi, lakini bado anahimiza msimamo kwamba njia nzuri na sahihi kwa wanasiasa kuwekana sawa, ni kukaa meza ya mazungumzo itakayojumuisha wadau wote ili kupata muafaka wa kitaifa.



Mwenyekiti wa TCD, James Mbatia. **PICHA: MTANDAO**

> Njia sahihi ya kutatua matatizo ya namna hiyo na kwa kawaida huanzia kwenye mazungumzo na kuishia katika makubaliano ya kindugu.

Akiwa na wanahabari jijini Dar es Salaam hivi karibuni, Mbatia anasema kwamba njia sahihi ya kutatua matatizo ya namna hiyo na kwa kawaida huanzia kwenye mazungumzo na kuishia katika makubaliano ya kindugu.

Mtazamo wa Mbatia, mwanasiasa aliyemo katika historia ya washiriki wa mstari wa mbele katika harakati za kisiasa kushinikiza mageuzi kuelekea vyama vingi vya siasa mwanzoni mwa miaka ya 1990, anatetea imani yake kwamba miaka 59 ya uhuru nchini, bado kuna baadhi ya mahitaji ya kidemokrasia.

Pia anakiri chama chake ni miongoni mwa vile ambavyo ndani ya miaka 28 vinaimba wimbo wa kudai katiba mpya na tume huru ya uchaguzi, hali inayoigharimu chama hicho kwa kiasi.

"Tunachoshauri ni sahihi kabisa, kwani hata nchi zilizoendelea zinatumia njia hiyo ya meza ya mazungumzo kwa ajili ya kumaliza tofauti za kisiasa kwa manufaa ya taifa husika," anasema.

Anashauri umuhimu wa wanasiasa kutetea na kuweka mbele taifa lao, badala ya vyama kwa kukubaliana kukaa meza moja ya mazungumzo, ili kutafuta muafaka na mbadala wa kususa tu au kujiweka pembeni.

"Kukutana katika meza ya mazungumzo kunasaidia kila chama kutoa dukuduku lake na hatimaye kufikia makubaliano ambayo msingi wake ni kuendelea kumlinda Mama Tanzania," anasema Mbatia.

Anafafanua suala la meza ya mazungumzo liliwahi kuhimizwa na Msajili wa Vyama vya Siasa, Jaji Mstaafu Francis Mutungi, baada ya CHADEMA kutaka kufanya maandamano ya nchi nzima Septemba mosi mwaka 2016.

Mbatia anendelea: "Lengo la maandamano yao lilikuwa ni kupinga hatua ya serikali kukataza kufanya mikutano ya kisiasa, lakini akashauri kuwapo kwa kikao cha pamoja kati yake na viongozi wa vyama vya siasa kupata muafaka," anasema.

Anasema, wakati CHADEMA wakiwa wamepanga kufanya maandamano waliyoita UKUTA, chama tawala CCM, kupitia Umoja wa Vijana (UVCCM), waliomba kibali cha kufanya maandamano kama hayo.

Mbatia anasema, ni katika mvutano wa aina hiyo na hatua ya namna hiyo, kambi ya upinzani nao ukasisitiza kufanya maandamano, licha ya katazo la serikali.

Ni Msajili wa Vyama vya Siasa, tena alipoamua kuitisha mazungumzo ya kupata maridhiano hali iliyosaidia kuwapo utulivu.

"Kwa mantiki hiyo, ni wazi busara ya kuitisha meza ya mazungumzo ni njia sahihi kukabiliana na mizozo kama hiyo inayotokana na uchaguzi mkuu hadi baadhi ya vyama kutopeleka bungeni wabunge wa viti maalum," anasema.

### YA BUNGENI

Mwenyekiti huyo anakumbushia mwaka 2016, hata Spika wa Bunge Job Ndugai, aliwahi kuwaita wabunge wa upinzani katika meza ya mazungumzo, baada ya kususia vikao vyake.

"Wakati akiitisha meza ya mazungumza alisema ili Bunge lifanye kazi yake, linahitaji kuishinda changamoto iliyopo ya Bunge kutokuwa kitu kimoja, huku akielezea chanzo kikuu kinachosababisha Bunge kusambaratika ni pamoja na 'u-vyama' kuzidi na wabunge kutojali maslahi ya Taifa," anasema.

Mbatia, anasema itakapotokea viongozi wa vyama vya siasa wanatoa uzito kwa suala la kukutana meza ya mazungumzo, itakuwa ni njia rahisi ya kuwekana sawa na kumaliza tofauti zilizopo miongoni mwa wanasiasa.

"Iwapo kila chama kitaendelea kuvutia upande wake bila kujali maslahi mapana ya Mama Tanzania, bado kutakuwapo na malalamiko yasiyofikia mwisho, ambayo huenda yangetatuliwa na meza ya mazungumzo," anasema.

# MWEZI JANUARI; MAMA MAJANGA SIASA AFRIKA

**INATOKA UK.11**

Badala ya kutoa heshima, alielekeza risasi kwa jemadari mkuu. Sababu inadaiwa ilikuwa kutiliana saini makubaliano ya amani na Israel mwaka 1979, ambayo yalisimamiwa na Rais Jimmy Carter wa Marekani, nchi anbayo tayari ilishaanza kuwa mfadhili muhimu wa Misri katika maeneo tofauti. Kundi kubwa la 'Udugu wa Kiislamu' lilichukia sana maamuzi hayo.

Nchini Misri, kuna historia inayodumu kuwa jeshi la Misri kwa takriban karne nzima iliyopita, lina kazi moja tu ya kupiga kundi la Muslim Brotherhood.

Hivyo, uhuru wa kisiasa ambao inapotokea kufanyika uchaguzi huru Misri, mtazamo mkuu ni kama vyama vyenye mrengo wa itikadi kali vitashinda, kisa kikuu ni kuchukia uwepo wa taifa la Israel.

Wayahudi kuhamia huko na kutaka kuunda nchi huru wanayotawala na kuwaondoa raia wa jadi eneo hilo, yaani Wapalestina imwebeba malalamiko makubwa.

Pia kuna mazingira ya kawaida ya rushwa katika serikali yoyote iliyoko madarakani, walio nje ya madaraka kudai wao hawatakuwa na simile na rushwa.

Baada ya Wayahudi kushinda vita dhidi ya nchi za Kiarabu zinazoizunguka pale Umoja wa Mataifa uliporidhia kuundwa kwa nchi hiyo mwaka 1947, kundi la Brotherhood lilimuelemea Mfalme Farouk wa Misri, wakidai amezembea vita.

Jawabu lao ilikuwa ni kuingia madarakani kwa utawala wa itikadi kali kumaliza suala la uvamizi wa Wayahudi eneo la Mashariki ya Kati na 'kuukomboa' mji wa Yerusalemu, na kimsingi bado ndiyo sera ya msingi ya Iran na makundi ya udugu wa kiitikadi kama Hamas na hata Al Qaeda ya marehemu Osama bin Laden.

Ili wasijazane bungeni na hatimaye kumwondoa mfalme, badala yake wanataka akae kiongozi wa kidini wa ngazi ya juu, kama marehemu Ayatollah Khomeini wa Iran na jeshi liliipindua nchi mwaka 1952.

Aliingia madarakani Kanali Gamal Abdel Nasser na Januari 1969 akafuatiwa na mwanafunzi wake, Kanali Muammar Gaddafi wa Libya, ambaye mfalme wake pia alikuwa anakaribia kuondolewa na makundi ya kiharakati.

Ni makundi hayo yaliyohochea uasi dhidi yake akafa Septemba 2011, akiwa anapeleka kikosi cha vifaru kuzima uasi jiji la Benghazi mashariki ya nchi hiyo.

Ufaransa ilihofia hatari ya umwagaji damu wa kutisha, ikaruhusu ndege za kivita za kusambaratisha mlolongo huo wa vifaru vikiwa njiani na punde ikagundua msafara mwingine wa magari kadhaa ya kijeshi ukienda mbio kusini, pia waliusambaratisha.

Kumbe ni Kanali Gaddafi alikuwa akikimbilia uhamishoni, akakamatwa hapo na akauawa baada ya muda mfupi.

RAIS SAHLE – WORK ZEWDE

# Mwanamama aliyekanyaga Tanzania juzi, amefungasha neema ushirikiano

**Na Christina Mwakangale**



Rais wa Ethiopia, Sahle-Work Zewde, alipokuwa na mwenyeji wake, Rais John Magufuli, alipompokea katika Uwanja wa Ndege wa Chato, mkoani Geita. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

RAIS wa Ethiopia, Sahle-Work Zewde, ni kati ya marais wanawake walioshika nafasi hiyo barani Afrika.

Zewde ambaye ni rais wa awamu ya tano tangu Oktoba 2018, ni kati ya marais wanawake wanne pekee barani Afrika waliowahi kushika wadhifa huo.

Kati yao waliokuwa marais ni Rais Ellen Johnson Sirleaf wa Liberia, Joyce Banda wa Malawi, Rais Saara Kuugongelwa-Amadhila wa Namibia na Rais Ameenah Gurib-Fakim wa Mauritius.

Pia historia inamwonyesha ni kati ya walioshika nyadhifa tofauti katika ngazi ya kimataifa ikiwamo Umoja wa Mataifa (UN).

Rais Zewde ambaye alifanya ziara ya kikazi ya siku moja hapa nchini, juzi, alipokelewa na mwenyeji wake Rais John Magufuli, wilayani Chato, mkoani Geita.

Katika hotuba yake Rias mwanamama huyo anasema uhusiano kati ya nchi mbili, Ethiopia na Tanzania, yametokana na waasisi wa mataifa hayo, Hayati HaileSelasse na Mwalimu Julius Nyerere, akiwataja kama mabingwa wa uafrika 'Pan-Africanism.'

Zilikuwa harakati zilizofanywa na watu walio na asili ya kiafrika duniani kuanzia karne ya 19, kuhimiza umoja na mshikamano, kupambana na utumwa na ukoloni.

"Nchi hizi ni kati ya waanzilishi wa Umoja wa Afrika, ukizungumzia kuanzishwa kwa umoja wa Afrika, huu huwezi kuacha kumtaja Dk. Salim Ahmed Salim, ambaye aliongoza umoja huu (iliyokuwa O.A.U) kwa vipindi vitatu, nikimtambua kama ni Muethiopia na rafiki wa kweli," anasema Rais Zewde.

Anasema Tanzania tangu miaka ya 1960 ikiwa na uhusiano na nchi hiyo, ni kati ya sababu ya kufunguliwa ubalozi wa Ethiopia, Dar es Salaam, Tanzania, miaka miwili iliyopita.

Rais Zewde anasema, nchi hiyo inaangazia fursa ya kibiashara zilizopo kati ya Ethiopia na Tanzania na katika mazungumzo ya kati ya Rais Magufuli na Rais Zewde.

Juzi walikubaliana mambo mbalimbali ikiwamo kuimarisha uchumi ushirikiano katika majeshi, huku Tanzania ikiahidi kupeleka walimu wa kufundisha lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Adis Ababa nchini Ethiopia.

Makubaliano mengine ni kuimarisha sekta ya mifugo, huku Tanzania ikiomba kujifunza kwa nchi hiyo ambayo inafanya vizuri na kufaidika na mifugo yake.

Wabunge nchini Ethiopia walimchagua Sahle-Work Zewde kuwa rais wa kwanza mwanamke Ethiopia.

**UZOEFU**

Rais Zewde ni mwanadiplomasia mzoefu, aliyewahi kuwa Balozi wa Ethiopia nchini Senegal na Djibouti. Pia aliwahi kushikilia nyadhifa kadhaa katika Umoja wa Mataifa (UN), ikiwamo Mkuu wa Ujenzi wa Amani katika Jamhuri ya Afrika ya Kati.

> Alichaguliwa kama rais wa kwanza mwanamke barani Afrika, mwaka 2005 miaka miwili baada ya kumalizika kwa vita vya wenyewe kwa wenyewe vya miaka 14, Liberia.

Kabla ya kuwa Rais wa Ethiopia, Juni mwaka 2018 Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), António Guterres alimteua Zewde kuwa Mwakilishi wa UN katika Umoja wa Afrika (AU).

Kwa mujibu wa katiba ya Ethiopia, Waziri Mkuu, yeye ndiye mtendaji na mkuu wa kiserikali, ikilinganishwa na wadhifa wa Rais, ilivyozoeleka kwingine.

Rais Zewde kwa sasa Waziri Mkuu wake ni Abiy Ahmed.

**KUCHAGULIWA KWAKE**

Rais Zewde alichaguliwa kuwa rais, wiki moja baada Waziri Mkuu, Abiy Ahmed kuteua Baraza la Mawaziri, huku nusu ya nyadhifa katika baraza hilo zikiwaangukia wanawake.

Rais Zewde, alichaguliwa baada ya kujiuzulu ghafla kwa kiongozi aliyekuwapo madarakani, Mulatu Teshome.

**MARAIS WANAWAKE**

Katika nchi 53 za Afrika, wanaoingia katika historia kuwa marais ni Rais wa Liberia, Ellen Johnson Sirleaf (72), aliyetajwa kama mmoja wa washindi wa tuzo ya amani ya Nobel mwaka 2011.

Alichaguliwa kama rais wa kwanza mwanamke barani Afrika, mwaka 2005 miaka miwili baada ya kumalizika kwa vita vya wenyewe kwa wenyewe vya miaka 14, Liberia.

Kiongozi mwingine, ni Joyce Banda aliyechaguliwa Malawi na mwanamke wa kwanza Kusini mwa Afrika, akiingia madarakani Aprili, mwaka 2012.

Alichukua urais wa Malawi kumrithi mtangulizi wake, aliyefariki.

Rais Saara Kuugongelwa-Amadhila, naye anaingia kwenye historia hiyo, baada ya aliteuliwa waziri mkuu wa Namibia, mwaka 2015, akiwa amewahi kuwa waziri wa fedha kwa miaka kadhaa.



Rais wa Ethiopia, Sahle-Work Zewde.

Akiwa ni mwanachama wa muda mrefu wa Chama cha South West Africa People's Organization (SWAPO), alikuwa uhamishoni Sierra Leone, akianza na chama hicho alikuwa na umri mdogo wa miaka 13.

Baada ya kuhitimu katika Chuo Kikuu Marekani, Kuugongelwa, alirudi Namibia na kufanya kazi kwa muda mfupi katika ofisi ya rais wa kwanza Sam Nujoma.

Nujoma, alimpandisha cheo kuongoza tume ya kitaifa ya mipango. Baada ya hapo alishikilia wadhifa wa waziri wa fedha, mwaka 2003 hadi alipopandishwa katika wadhifa wa waziri mkuu na rais Hage Gottfried Geingob.

Pia kuna mwanamke Meenah Gurib-Fakim wa Mauritius, ambaye hata hivyo alijiuzulu, kutokana na mzozo wa kifedha uliokuwa unamkabili.

Alituhumiwa kutumia kadi ya fedha aliyopewa na shirika la misaada kununua vitu vya binafsi vyenye thamani kubwa.

Rais Gurib-Fakim ni mwanasayansi na mwaka 2015 alikuwa mwanamke wa kwanza kuchaguliwa katika wadhifa wa rais wa Mauritius.

**FURSA ETHIOPIA**

Nchi ya Ethiopia ni nchi ya kwanza kuwa na idadi kubwa ya mifugo barani Afrika, pia ina uzalishaji mkubwa wa maziwa.

Kwa mujibu wa utafiti uliofanyika katika nchi mbalimbali barani na taasisi zilizotafiti, ikiwamo ILRI na Shirika la Chakula Duniani (FAO), ilipotoa orodha ya nchi 10 zinazoongoza kwa ufugaji na uzalishaji wa maziwa.

Katika uzalishaji wa maziwa, Ethiopia inazalisha wastani wa lita bilioni 4.39 kwa mwaka, kutoka kikiwa na idadi ya ng'ombe wa maziwa milioni 9.6.

Aidha, limetengwa eneo la kilomita za mraba 700,000 ambazo hutumiwa na wafugaji kwa ajili ya malisho.

# HUYU NDIYE LUCY LAMECK

## • Kijana jembe la TANU kabla uhuru • Alikataa uuguzi uliojaa staili ukoloni • Waziri mwanamke wa kwanza nchini • Bungeni 'ngoma droo' na kina baba • Mwezeshaji wa kitenge vazi la taifa • Alikuwa mbele kusukuma 'operesheni kukabili mafataki'

**Na Mwandishi Wetu**

LUCY Lameck, kupewa jina la mtaa; bado ni mwendelezo wa kukumbukwa kama mwanamke aliyetoa mchango mkubwa katika harakati za kupigania Uhuru wa Tanganyika, akiungana na kinamama magwiji kama maarufu Bibi Titi Mohamed.

Leo hii, sifa zake hizo zinamfanya mama huyo kuwa mwanasiasa na mwanaharakati maarufu, ikiwamo kuupinga ukoloni wa Kiingerezare na dhana nzima ya ubaguzi, akiwa mtetezi mkubwa wa wanawake.

Ni suta hiyo ya ushujaa leo hii, umeifanya Ujerumani kubadili jina la mtaa wa Wissmann na kupewa jina la Mtanzania huyo.

**UHURU WA NCHI**

Katika siasa za Tanganyika kabla na baada ya uhuru wa nchi mwaka 1961, jina la Lucy Lameck liliingia katika kundi la wanasiasa maarufu kama Oscar Kambona, Lawi Sijaona, Nsilo Swai, Saidi Tewa na wengine walikuwa katika Baraza la Mawanziri la kwanza la Tanganyika na baadaye Tanzania.

Pia, ni wakati huo alikuwa sehemu ya viongozi wa juu wa Umoja wa Wanawake (UWT), akipewa sifa za kujiamini kiasi cha kukabiliana na wanasiasa wanaume katika kile kinachojulikana sasa kwa jina la 'mfumo dume.'

**HARAKATI ZAKE**

Chama cha TANU chini ya waasisi wake wa wakati huo, kiliendesha harakati za kudai uhuru wa nchi dhidi ya Ukoloni wa Uingereza. Hapo ndipo kilipoibua jina la Lucy Lameck.

Baada ya kumaliza mafunzo ya uuguzi mwaka 1950, Lucy alikataa kufanya kazi katika mfumo wa matibabu wa kikoloni wa Uingereza na kuchagua kufanya kazi ya ukarani.

Katika kitabu cha 'Nyerere and Africa: End of an Era', mwandishi Godfrey Mwakikagile anaeleza katoka nukuu "Tawi la TANU Moshi lilipofanya mkutano wake wa kwanza, mmoja wa wahudhuriaji alikuwa mwanamke kijana aliyeitwa Lucy Lameck."

Akitokea katika familia ya wakulima nyumbani kwao Moshi ndani ya umri wake kijana. Lucy hakuachwa tena nyuma katika vuguvugu na mapambano ya kudai uhuru.

Mwanahistoria Mohammed Said, anaeleza umuhimu wa Lucy Lameck, wakati huo katika harakati za TANU, akitamka: "Alikuwa mwanamke msomi ndani ya TANU. Kwa kushirikiana na wanawake wengine Halima Selengia, Amina Kinabo, Mama Binti Maalim waliifanya TANU kuwa na nguvu Moshi".

Mohammed anaendelea: "Katika matawi yote ya TANU Tanganyika, hakuna tawi lililopata nguvu kutoka kwa wanawake kama tawi la Moshi Mjini. Kinamama hao walileta ngoma ya Msanja ambayo ilichangamsha chama".



Lucy Lameck. **PICHA: MTANDAO**

Baadae Lucy alipata ufadhili na kwenda kusoma katika Chuo cha Ruskin, Oxford, Uingereza na chuo kingine huko Michigan, Marekani kabla ya kurudi Tanzania na kuingia katika siasa moja kwa moja.

**FALSAFA YAKE**

Lucy alikuwa mpinzani wa wazi dhidi ya ukoloni na hata alipohojiwa na habari kuchapishwa Febuari 1960, kwenye jarida la Jet la nchini Marekani, ikiwa mwaka mmoja na miezi minane kabla ya uhuru wa nchi, Lucy aliulaumu ukoloni kuwa chanzo cha umaskini uliokuwapo Tanganyika.

Katika ufafanuzi wake, Lucy aliuponda ukoloni wa Uingereza kwa kauli yenye ishara ya dhamira "utaondoshwa na kurudishwa England (Uingereza) hivi punde."

**BAADA YA UHURU**

Mwaka 1961, Lucy aliingia kwa mara ya kwanza katika Bunge la Tanganyika, alipoteuliwa baada ya kuteuliwa na Waziri Mkuu wakati huo, Julius Nyerere kuwa mbunge, kabla ya kuchaguliwa na wananchi katika Bunge la kitaifa la mwaka 1965.

Mwaka 1962 aliandika historia ya kuwa mwanamke wa kwanza kuteuliwa kuwa Waziri, akishika nafasi ya Waziri Mdogo wa Maendeleo ya Jamii na baadaye aliteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Afya, kati ya mwaka 1967 hadi 1972.

Mwanasiasa mkongwe nchini na Spika wa Bunge mstaafu, anamkumbuka Lucy akiwa Bungeni kwamba: "Alikuwa mwanamke mwenye ujasiri na uthubutu, kwa sababu wakati ule haukuwa mwepesi kwa mwanamke".

Anakumbukwa kwa uanaharakati wa kupiga vita mila na desturi zilizokinzana na haki na usawa wa kijinsia, akilenga umuhimu na ubora wa wanawake katika maisha mara baada ya uhuru wa nchi.

Sehemu ya hoja zinazotajwa zina shinikizo lake kwa kushirikiana na kinamama wenzake bungeni, ni pamoja na dai la kupitishwa sheria dhidi ya wanaume wanaowapa mimba watoto wasichana walipe faini, wafungwe na kutunza watoto.

Pia, anatajwa kuwa mstari wa mbele kulaani kitendo cha kuwafukuza shule wasichana waliopata mimba na kuna kipindi alikuwa mstari wa mbele kudai kitenge kuwa vazi la taifa kwa wanawake wa Tanzania.

Kwa mujibu wa maoni ya mwaandishi habari mkongwe na mchambuzi Mohammed AbdulRahman anaeishi Ujerumani kwa muda mrefu ni kwamba; "uamuzi huo una lengo la kufuta historia mbaya ya Utawala wa Ujerumani katika Tanganyika".

Wachambuzi wanaashiria kwamba hatua ya kubatiza mtaa wa Berlin, jina la Lucy Lameck una maana pana sana, kwani itakuza utalii wa nchi kwa wengi zaidi.

Inaelezwa kwamba, litaweza kuwakumbusha wahusika juu ya haja ya kuwapa heshima inayostahiki mashujaa sio tu wa kisiasa, pia katika harakati nyinginezo za kijamii, ambazo wengi wamesahauliwa katika historia muhimu .

Lucy Selina Lameck Somi, alizaliwa mwaka 1934 na kuaga dunia Machi 1993.

***Kwa mujibu wa BBC.***





# EWURA yatakiwa kudhibiti matumizi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imetakiwa kukabiliana na uzembe, rushwa na matumizi yasiyo na lazima mahala pa kazi ili kuongeza tija.

Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, alitoa kauli hiyo jana jijini hapa alipokuwa akizindua baraza la kwanza la wafanyakazi wa mamlaka hiyo.

Alisema ni wajibu wa kila mfanyakazi wa EWURA kuhakikisha anaondoa hali hiyo ili kutekeleza malengo yaliyopangwa kwa wakati.

"Vile vile hakikisheni mnatunza mali na vifaa mlivyokabidhiwa kufanyia kazi, pamoja na kufika kazini na kuondoka kwa muda uliopangwa, nisisitize kwanza uwajibikaji, hii ni nguzo kuu ya mafanikio katika sehemu yoyote ya kazi," alisema.

Alitaka mamlaka hiyo kutoa ushirikiano kwa watumishi ili kuondoa malalamiko na kushughulikia masuala ya maendeleo kwa wakati.

"Wajumbe mnaowakilisha wafanyakazi wote wa EWURA, hamna budi kuwa mfano katika jambo hili la uwajibikaji na kuleta ufanisi, nimeambiwa kutakuwa na mada zitakazowasilishwa kuhusu mabaraza ya wafanyakazi na vyama vya wafanyakazi hususani TUGHE," alisema.

Alisisitiza kila mjumbe wa baraza hilo kutimiza wajibu wake.

"Naamini sote tukifanya kazi zetu kwa umakini tutaweza kutoa mchango wetu kikamilifu katika kufikia malengo ya serikali ya awamu ya tano ya ujenzi wa uchumi wa viwanda na katika kukamilisha azma hiyo, watumishi wa EWURA wanaowajibu mkubwa wa kuongeza kujituma na kuwa waadilifu," alisema.

Alisema mabaraza ya wafanyakazi yameanzishwa kisheria ili kusimamia haki na ustawi wa wafanyakazi mahali pa kazi.

"Ni matarajio yangu kila mjumbe wa baraza atatimiza wajibu wake na kufanikisha azma ya serikali ya awamu ya tano, muongeze kujituma na kuwajibika, tuendelee kufanya kazi kwa ubunifu na yale yote yanayopaswa kusimamiwa kwa ubora yafanyike," alisema.

Kwa upande wake, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Godfrey Chibulunje, alisema baraza hilo ni la kwanza kufanyika kwenye mamlaka hiyo ambalo linalenga kujadili masuala mbalimbali ikiwamo kuhakikisha huduma za udhibiti wa nishati na maji zifanyike kwa ubora unaotakiwa.

# Waziri ataka uchunguzi bei ya tumbaku

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Kilimo, Profesa Adolf Mkenda, ameiagiza Bodi ya Tumbaku kuchunguza sababu za tumbaku ya Tanzania kuuzwa kwa bei kubwa Zambia, huku nchini ikiuzwa kwa bei ndogo.

Akizungumza na waandishi wa habari, Profesa Mkenda alisema tumbaku inayouzwa Zambia ni ile inayobaki baada ya kuuza kwa mkataba katika kampuni za ununuzi.

Alisema mabaki hayo ambayo ni bora huitwa makinikia na hununuliwa na kampuni hizo kwa bei ndogo nje ya mkataba na kuuzwa nchini humo kwa bei kubwa.

Profesa Mkenda alisema Tanzania ni nchi ya 10 duniani kwa kulima tumbaku, lakini cha kushangaza nchini inauzwa kwa bei ndogo na ikipelekwa Zambia inauzwa kwa bei ya juu.

"Hiki kitu kinanishangaza sana, na ndio maana nimeagiza Bodi ya Tumbaku kuhakikisha inachunguza ili mkulima na taifa waweze kufaidika na zao hilo," alisema Profesa Mkenda.

Hata hivyo, alisema bado kuna mfumo mbaya wa wanunuzi wa tumbaku nchini na kusababisha tumbaku kuuzwa nje kwa gharama kubwa. Aliitaka bodi hiyo kuchunguza na kutoa majibu haraka.

Vile vile, alisema serikali kwa kushirikiana na wadau imeweka mkakati wa kutafuta soko la tumbaku katika nchi za kiarabu na nyingine, ili kuinua pato la taifa na kuwasaidia wakulima.

Alisema zao hilo lina soko katika nchi za China, Misri, Sudani, Algeria, Indonesia na nyingine.

Kadhalika, alisema serikali kwa kushirikiana na wadau wameanza jitihada za kufufua kiwanda cha tumbaku cha Morogoro na Songea mkoani Ruvuma



Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Innocent Bashungwa, akiwasilisha maelezo kuhusu muundo na majukumu ya wizara yake, mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, jijini Dodoma jana. Kushoto kwake ni Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Hassan Abbas. **PICHA: BUNGE**.

# Watumishi wabadhirifu kushughulikiwa

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, amemwagiza Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Doto James, kuwashughulikia watumishi wazembe, wavivu na wabadhirifu wa fedha za umma.

Akifungua Baraza la Wafanyakazi wa wizara hiyo, Dk. Mpango alisema watumishi hao hawastahili kuwa kwenye wizara hiyo.

"Nakuagiza Katibu Mkuu usisite kutumia mamlaka uliyonayo kisheria kuchukua hatua kali dhidi ya watumishi wa aina hiyo," alisema.

Aliwataka kufanya kazi kwa weledi ili kuharakisha maendeleo ya nchi kwa kuwa serikali bado ina kazi kubwa ya kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati kama ujenzi wa reli ya kisasa (SGR).

Aliwaonya watumishi hao kuacha kutoa siri za serikali na watakaobainika watachukuliwa hatua.

Alisema mtumishi yeyote atakayebainika kukiuka taratibu, miongozo na miiko ya utunzaji siri hizo atajutia ukaidi wake.

"Natanguliza onyo kali kwa mtumishi yeyote atakayebainika kukiuka taratibu, miongozo na miiko ya kazi yake ndani ya Wizara ya Fedha na Mipango utajutia ukaidi wake, napenda pia kutumia nafasi hii kuwakumbusha viapo vyetu vya kutunza siri katika nafasi zetu mbalimbali tulizopewa kusimamia," alisema.

Alibanisha kuwa utandawazi na matumizi huria ya teknolojia ya habari ni tatizo kubwa la utunzaji wa siri za ofisi na taarifa nyeti za serikali.

Aliwakumbusha wafanyakazi hao kuwa wana majukumu makubwa katika mstakabali wa taifa hasa wakati huu wa kutekeleza bajeti ya serikali, huku kukiwa na msukosuko wa kiuchumi duniani unaotokana na ugonjwa wa corona.

Mwenyekiti wa Baraza hilo, Doto James, alisema mkutano huo utakuwa na jukumu la kuwachagua viongozi wapya pamoja na kuwasilishwa kwa mada mbalimbali.

Aliwapongeza wafanyakazi wa wizara hiyo kwa kufanyakazi kwa bidii na kufanikisha nchi kuingia kwenye uchumi wa kati kabla ya malengo yaliyokusudiwa ya kuingia huko mwaka 2025.

# Wazazi kushurutishwa kutoa chakula shuleni

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI mkoani Mbeya, imetishia kutumia vyombo vya dola kuwashurutisha wazazi wa wanafunzi wanaosoma katika Shule ya Sekondari Iyela iliyopo jijini hapo, kutoa chakula cha mchana kwa watoto wao ikiwa ni miongoni mwa mikakati ya kuinua kiwango cha elimu.

Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mbeya ikiambatana na maofisa mbalimbali wa Jiji la Mbeya, ilifanya ziara ya kushtukiza hivi karibuni na kubaini katika shule hiyo ambayo ni miongoni mwa shule zilizokuwa na matokeo mabovu ya kidato cha nne mwaka uliopita yaliyotangazwa hivi karibuni.

Kamati hiyo ilibaini kuwa nidhamu ya wanafunzi wa shule hiyo ni mbovu na hata walimu wao hawawasimamii ipasavyo kutokana na makundi yote kuingia shuleni kwa kuchelewa kinyume na taratibu na miongozo ya elimu nchini.

Kufuatia hali hiyo Mwenyekiti wa Kamati hiyo ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, aliwaamuru wanafunzi wote kuja na wazazi kwa ajili ya kikao maalumu na viongozi wa serikali na kikao hicho kilifanyika juzi shuleni hapo.

Chalamila alisema amelazimika kuwalazimisha wazazi hao kupeleka chakula kwa wanafunzi baada ya kubaini wameshindwa kutimiza wajibu huo kwa njia ya amani licha ya kupatiwa maelekezo na kuelimishwa faida ya utaratibu huo.

"Sasa inaonyesha kuwa taaluma kidemokrasia mmeshindwa, sasa nawapa wiki moja mjitafakari, baada ya hapo hivi vyombo vya dola vitawashughulikia na wala siwatanii kabisa," alisema Chalamila.

Alisema kwa sasa serikali inakusudia kuzifanya shule zote za sekondari za mjini kuwa za bweni kwa kujenga hosteli na ili kufanikisha zoezi hilo la uboreshaji wa elimu.

Ofisa Elimu wa Mkoa wa Mbeya, Majuto Njanga, alisema mwaka huu jumla ya wanafunzi 664 wamepangiwa kuanza kidato cha kwanza katika shule hiyo, lakini mpaka sasa ni wanafunzi 200 pekee ndio walioripoti na kuanza masomo na wengine hawajulikani walipo.

Alisema serikali imeshatimiza wajibu wake kwa kujenga miundombinu ya elimu ikiwamo vyumba vya madarasa, vyoo, maabara na ofisi za walimu na kwamba hakuna sababu ya wazazi kutowapeleka watoto wao shuleni.



Wakazi wa Kijiji cha Mapogoro katika Wilaya ya Mbarali, mkoani Mbeya, wakimzika kijana Pawa Sama (22) mkazi wa kijiji hicho, aliyejinyonga baada ya ng'ombe wake zaidi ya 50 kukamatwa na vikosi vya serikali ndani ya Bonde la Ihefu wilayani humo. **PICHA: NEBART MSOKWA**.

# Operesheni tokomeza mifugo hifadhini yafanikiwa

**Na Nebart Msokwa, MBARALI**

OPERESHENI tokomeza mifugo ndani ya Bonde la Ihefu lililopo ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, wilayani Mbarali katika Mkoa wa Mbeya, imezaa matunda baada ya zaidi ya ng'ombe 200 kukamatwa na vikosi vya ulinzi na usalama.

Operesheni hiyo ilianza kutekelezwa juzi baada ya siku sita zilizotolewa na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, kwa wafugaji waliovamia bonde hilo kuondoa mifugo yao kwa hiari ndani ya bonde hilo kuisha.

Mkuu wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Uhifadhi, Izumbe Msindai, alisema baada ya agizo la Mkuu wa Mkoa, asilimia 90 ya wafugaji waliondoa mifugo yao na wachache waliokaidi mifugo yao ilikamatwa.

Alisema vikosi vya majeshi vilifanya doria kwenye maeneo mbalimbali ya bonde hilo na kukuta makundi matatu ya mifugo yakiwa hayajaondolewa na kuamua kuyaweka chini ya ulinzi.

"Kuna hawa ambao wapo hapa pembezoni mwa mto wapo 120, kuna 46 ambao wapo sehemu nyingine na wengine wapo kule Ikoga, lakini ukilinganisha idadi ya ng'ombe waliokamatwa na makundi yalivyokuwa unagundua tumefanikiwa kwa kiasi kikubwa," alisema Msindai.

Alisema msako bado unaendelea kwa madai kuwa baadhi ya wafugaji hao huwa wanaondoa mifugo hiyo kwa muda na kuirejesha baada ya kubaini kuwa ufuatiliaji umepungua.

Mkuu wa Ikolojia wa uwapo wa mifugo ndani ya bonde hilo una madhara ya kiikolojia kutokana na bonde hilo kuwa miongoni mwa chanzo kikubwa cha Mto Ruaha Mkuu.

Alisema mifugo hiyo inaharibu chanzo hicho na kuufanya mto huo kutokuwa na uwezo wa kutiririsha maji mwaka mzima hali inayoathiri viumbe wanaoishi kwa kutegemea mto huo pamoja na shughuli zingine za kiuchumi.

Alisema kuanzia mwaka 1995 wafugaji hao walipoanza kuvamia bonde hilo, Mto Ruaha umekuwa ukikauka kwa kipindi cha kati ya miezi miwili mpaka mitano kila mwaka tofauti na ilivyokuwa awali ulikuwa ukitiririsha maji mwaka mzima.

"Uharibifu wa mto huu una athari sio kwa wanyama pekee bali hata kwa binadamu, lakini kama mnavyoona mazingira yameharibiwa vibaya, madhara yake hayako kwa wanyama pekee bali hata sisi binadamu tunaathirika," alisema Chalamila.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, alivitaka vikosi hivyo kuendelea na operesheni hiyo ili kuhakikisha eneo lote la hifadhi linabaki bila mifugo na badala yake wabaki wanyamapori pekee.

# Wajasiriamali walia kukwamishwa na wakopaji

**Na Grace Mwakalinga, KYELA**

MABINTI wajasiriamali kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Kyela na Jiji la Mbeya, wamesema miongoni mwa vikwazo vinavyosababisha washindwe kutimiza azma yao ya kujikwamua kiuchumi ni wakopaji kushindwa kurejesha kwa wakati na ukosefu wa mitaji.

Waliyaeleza hayo jana, wakati wa mafunzo ya kuwajengea uwezo yaliyoandaliwa na Taasisi ya Tanzania Data Lab (Dlab), ambayo yanaendeshwa kwa kushirikiana na Shirika la PEPFAR ili kuwajengea uwezo wajasiriamali mabinti waweze kujikimu kiuchumi na kuondokana na mambo yatakayochangia kujiingiza kwenye vishawishi vya maambukizi ya virusi vya Ukimwi.

Mmoja wa wajasiriamali hao, Shukuru Mwakamala, kutoka Kata ya Iganjo, alisema anakabiliwa na vikwazo vingi kwenye biashara yake ya ununuzi wa mboga na matunda.

Vikwazo hivyo ni wateja wanaokopa kushindwa kurejesha fedha kwa wakati sambamba na ukosefu wa mitaji katika kuendesha biashara.

Alisema biashara yake ya matunda na mboga ambayo ananunua kutoka Wilaya ya Rungwe na maeneo mengine ya Mkoa wa Rukwa licha ya wateja kukopa na kutorejesha fedha kwa wakati, lakini hakuna wateja wa kutosha kuwauzia kutokana na hali ya maisha ilivyo sasa.

"Moja ya vikwazo tunavyokabiliana navyo ni mitaji, mabinti tuna nia ya kujikwamua kiuchumi, lakini vikwazo ni vingi ikiwamo mitaji hali inayosababisha bidhaa wanazoziuza kutokuwa na faida, lingine ni wateja kukopa na kushindwa kurejesha fedha," alisema Mwakamala.

Baitha Mwangosi, kutoka wilayani Kyela, anayejishughulisha na uuzaji wa genge na viatu vya kimasai, alisema kikwazo kinachomfanya ashindwe kufikia malengo ni mazingira ya kibiashara yalivyo ambayo yanachangia kukosa wateja wa kutosha.

Akizungumzia mafunzo hayo, Mratibu wa Mafunzo, Somoe Mkwachu kutoka Taasisi ya Tanzania Data Lab (Dlab), ambao wanaendesha Programu ya Data4Her wamejikita kuwajengea uwezo mabinti namna ya kuendesha biashara zao kwa kutumia data.



# Mwinyi awapa mtihani makatibu wakuu

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amewataka makatibu wakuu wapya kutekeleza majukumu yao ipasavyo ikiwamo kuzisimamia fedha za serikali ili kupambana na uzembe na ufisadi.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo juzi katika viwanja vya Ikulu Zanzibar, baada ya kuwaapisha viongozi mbalimbali aliowateua hivi karibuni, wakiwamo makatibu wakuu.

Alisema ameamua kupunguza idadi ya manaibu makatibu wakuu kwa lengo la kupunguza ukubwa wa serikali pamoja na kupunguza matumizi.

Alisema makatibu wakuu ndio maofisa masuuli ambao ni wasimamizi wa fedha za serikali, ambapo aliwataka kuhakikisha fedha za maduhuli za serikali zinapatikana kwa kuwa kuna taasisi zinakusanya kwa kutumia risiti za mkono, na kuagiza fedha kukusanywa kwa mtandao.

Aliwataka kuondoa matumizi yasiyokuwa na tija kama vile semina na makongamano na kuwataka kuondoa aina zote za ubadhirifu, matumizi nje ya bajeti kwani mifumo ya bajeti ya fedha za serikali zimekuwa zikichezewa sana.

Alisema hali hiyo imesababisha wahasibu kadhaa kuuchezea mfumo huo na kuchukua fedha nyingi na kusema ameshaagiza wahasibu wote waliotuhumiwa kufanya mchezo huo kusimamishwa kazi kati ya wahasibu zaidi ya 80 ambao walikuwa serikalini.

Aliutaka uongozi wa Wizara ya Fedha kurekebisha mfumo huo mara moja, huku akiwataka makatibu wakuu hao kuyafanyia kazi mambo hayo ili kuhakikisha fedha za serikali zinatumika katika mambo yaliyokusudiwa badala ya kutumika ovyo nje ya bajeti.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akiwa na Makamu wake wa Kwanza, Maalim Seif Sharif Hamad na Makamu wake wa pili, Hemed Suleiman Abdalla, na viongozi wa serikali baada ya kuwaapisha makatibu wakuu na manaibu, katika viwanja vya Ikulu, Zanzibar juzi. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Malori ya mchanga yatangaziwa kiama

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MKUU wa Wilaya ya Kaskazini 'B', Aboud Hassan Mwinyi, amesema atawachukulia hatua za kisheria madereva wa magari ya mchanga ambao wamekuwa wakikaidi maagizo yanayotolewa na serikali kuhusu uchimbaji katika maeneo yasiyo rasmi.

Madereva hao wanadaiwa kutoa kisingizio cha kuuziwa maeneo hayo na wamiliki wa mashamba.

Amesema hivi karibuni alifanya ziara katika maeneo yanayochimbwa mchanga kiholela na kuwakataza madereva hao kuacha tabia ya kuchimba mchanga katika maeneo yasiyo rasmi, lakini bado wameonekana kukaidi maelekezo hayo, hali ambayo inasababisha kutokea kwa uharibifu wa mazingira.

Akizungumza na madereva, wamiliki wa mashamba na wamiliki wa magari ya mchanga huko Mahonda, Aboud alisema ili kuzuia vitendo hivyo, ni vyema kwa wamiliki wa mashamba kuacha tabia ya kuuza maeneo yao bila ya kufuata taratibu zilizowekwa na serikali pamoja na kuahidi kufanya ziara za mara kwa mara katika maeneo yanayojihusisha na vitendo hivyo ili kulinda mazingira.

Alisema serikali itazidi kuwa kali kwa kuwachukulia hatua za kisheria kwa wale wote wanaozivunja sheria zilizowekwa kwa makusudi ili kuharibu mazingira.

Alisema serikali ilikuwa ikipiga kelele juu ya utunzaji wa mazingira hususani suala la uchimbaji wa mchanga kiholela.

"Suala la kuchimba mchanga kiholela halikubaliki, huu ni uharibifu wa mazingira tena mkubwa ikiangalia sasa hivi dunia inakabiliwa na mabadiliko ya tabianchi, hivyo wananchi mnatakiwa kutoa taarifa katika vyombo husika ili kukomesha vitendo hivi katika maeneo ambayo hayapo kisheria kuendesha shughuli hizo," alisema.

Hata hivyo, Aboud amewataka wachimbaji wa mchanga kuwa wastaamilivu kwani serikali imeandaa eneo lingine na kilichobaki ni kuboresha miundombinu ya eneo hilo ili liweze kufanya kazi.

Mapema akitoa maelezo kwa Mkuu wa Wilaya, msimamizi wa shimo la mchanga, Pangatupu Hassan Is-haka Bakar, aliwataka madereva hao kufuata taratibu za serikali ili kuzuia migogoro kwa wananchi.

Wamiliki wa magari walikiri kuhusika na uchimbaji wa mchanga kinyume cha utaratibu na kuiomba serikali kufanya jitihada za haraka ili kufungua shimo lingine la mchanga kwani maisha yao yanategemea shughuli hiyo.

Kikao hicho kiliitishwa baada ya kukamatwa kwa magari ya mchanga Bumbwini Mafufuni Jumamosi ambapo madereva tisa wamefikishwa katika Kituo cha Polisi Mahonda.

# ...Wafukuzwa eneo la Mwanakwerekwe

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MADEREVA wanaojishughulisha na biashara ya mchanga, mawe, kifusi na kokoto wametakiwa kuondoka katika eneo la Mwanakwerekwe na kwenda kuendelea na biashara hizo katika eneo lililotengwa na serikali.

Akizungumza na madereva hao, katika eneo la Mwanakwerekwe Mkuu wa Wilaya ya Magharibi 'B', Hamida Mussa Khamis, alisema serikali imeshapanga eneo maalum kwa ajili ya biashara hizo huko Jumbi, hivyo wanapaswa kutii agizo hilo la kwenda kuendelea na biashara hizo katika eneo lililopangwa.

Alisema kuwa Serikali ya Wilaya itasimamia kuhakikisha eneo jipya walilopangiwa linafanyiwa marekebisho, hivyo amewasihi wafanyabiashara hao kufuata maagizo ya serikali.

Alisema kumekuwapo na tabia ya baadhi ya madereva hao kuweka magari ya mawe na mchanga sehemu mbalimbali za wilaya hiyo, hivyo ni vyema wakarudi katika eneo ambalo serikali imelitenga.

"Kila sehemu ya wilaya au mji huu wa Zanzibar utakuta magari ya mchanga wakiendesha shughuli zao... hii jamani ni uchafu, na wakati kuna eneo maalum serikali imelitenga, hivyo naomba turudini katika eneo mlilotengewa," alisema.

Madereva hao walisema eneo lililotengwa kwa ajili ya kufanyia biashara zao, kuna changamoto ambazo ni vyema serikali ikazifanyia utatuzi ili waweze kufanya shughuli za biashara hizo katika eneo hilo.

Naye Mkurugenzi wa Manispaa ya Wilaya ya Magharibi 'B', Ali Abdallah Natepe, alisema wameshafanya tathmini ya marekebisho ambayo wafanyabiashara hao wamekuwa wakiyalalamikia katika eneo hilo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA SHULE

Keland Nursery and Primary School iliyopo Salasala Rtd inatangaza Nafasi Za Awali Na Msingi. Mawasiliano : 0713327613.

**Uza,**
**Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**
**Tupigie 0782253676**

## KUPOTEA KWA CHETI



**OMARY .S. WAWA** anatangaza kupotelewa kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1194/0064-2014** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary **BISMARCK** mwaka **2014**,yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi **Polisi taarifa KUMB.NA.DOM/B.I/21/VOL.IX/421**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**HARSUKH RAMNIKLAL DUBAL** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 714 DLM TOYOTA HARRIER.** Chassis namba **MCU300008508.** Engine namba **IMZ1753603.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **DAR/URA/RB/45915/2021.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**EMMA GEORGE MBWAMBO** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 973 AMG TOYOTA CANTER.** Chassis namba **FE425E54065.** Engine namba **4D32829527.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **DAR/URA/RB/45909/2021.**

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako la
Nipashe kila siku

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Waasi 44 CAR wauawa

**Bangui,** CAR

JESHI la Jamhuri ya Afrika ya Kati, FACA na vikosi vya washirika wamefanya shambulio karibu na kijiji cha Lambi na kwamba waasi 44 waliuawa.

Kulingana na mamlaka, watu 44 waliuawa upande wa waasi wa CPC baada ya shambulio la Jumapili.

Pia mamlaka ilisema, wafungwa watatu walisafirishwa kwenda katika mji mkuu wa nchi hiyo, Bangui.

Vikosi vya Jeshi vya Afrika ya Kati vilichukua udhibiti wa mji wa Boda, ulioko kilomita 180 Kusini Magharibi mwa Bangui katika mkoa wa Lobaye, ambako waasi wa CPC walikuwa wamepiga kambi kwa zaidi ya mwezi mmoja.

Jamhuri ya Afrika ya Kati (CAR), imeendelea kukumbwa na mapigano kati ya vikosi vya serikali na makundi ya waasi, tangu kuanza kwa mchakato wa uchaguzi nchini humo.

Rais wa zamani wa CAR, François Bozize, ameendelea kunyooshewa kidole cha lawama kwamba anahusika katika kuhatarisha usalama wa nchi hiyo. **RFI**



Maelfu ya wakulima wakikabiliana na polisi nchini India, walioandamana jana kudai mabadiliko kwenye sekta ya kilimo wakiingia katika uwanja wa kihistoria wa Red Fort katika mji mkuu, New Delhi. **PICHA/BBC**

# Mashtaka dhidi ya Trump yatua seneti

**Washington,** MAREKANI

BARAZA la Wawakilishi la Bunge la Marekani, limewasilisha hati ya mashtaka mbele ya Baraza la Seneti dhidi ya rais wa zamani Donald Trump na kufungua njia ya kuanza kwa shauri la pili la kihistoria.

Wawakilishi tisa walioteuliwa kuongoza mchakato huo wamewasilisha shtaka moja pekee linalomtuhumu Trump, kuchochea uasi baada ya wafuasi wake kuvamia majengo ya Bunge mjini Washington, mapema mwezi huu.

Wawakilishi hao waliwasilisha hati ya mashtaka mbele ya Baraza la Seneti na kufungua shauri kwa kiongozi wa taifa hilo, kushtakiwa mara mbili na Bunge.

Mwakilishi wa Jimbo la Maryland, Jamie Raskin ndiye alisoma shakta dhidi ya Trump ndani ya ukumbi wa Baraza la Seneti.

Kuwasilishwa kwa hati hiyo ya mashtaka iliyoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi linaloongozwa na Chama cha Democrat, Januari 13, mwaka huu, kunafungua njia ya kuanza kwa shauri dhidi ya Trump.

Kiongozi wa walio wengi katika Baraza la Seneti, Chuck Schumer alisema wajumbe 100 wa baraza hilo ambalo watafanya kazi kama mahakimu walioapishwa jana. Tayari wito wa kufika mbele ya baraza umetumwa kwa Trump.

Wanasiasa wa Democratic na Republican walikubaliana kuchelewesha kwa muda wa wiki mbili kuanza kwa shauri hilo, ili kumruhusu Trump kuandaa utetezi wake dhidi ya shtaka linalomkabili. Shtaka hilo ni kuchochea uasi na kuruhusu Baraza la Seneti kuidhinisha wateule wa nafasi mbalimbali za utawala, Rais Joe Biden.

Kesi hiyo itaongozwa na Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Seneti, Patrick Leahy kutoka Chama cha Democratic ambaye ni seneta mkongwe zaidi badala ya Jaji Mkuu wa Marekani, John Roberts aliyeongoza shauri la kwanza dhidi ya Trump wakati alipokuwa rais. **DW**

## Mlipuko waua wawili Syria

**Tel Abyad,** SYRIA

RAIA wawili wameuawa na wengine kujeruhiwa katika mlipuko wa bomu lililotegwa kwenye pikipiki katika Wilaya ya Tal Abyad, ambayo iko chini ya udhibiti wa wapinzani Kaskazini mwa Syria.

Waliojeruhiwa vibaya walipelekwa Uturuki kwa matibabu zaidi.

Vikosi vya usalama vya mitaa, ambavyo vilichunguza eneo hilo, vinasisitiza uwezekano wa kuwa shambulizi hilo lilitekelezwa na kundi la kigaidi la YPG / PKK.

Wilaya ya Tel Abyad Kaskazini, ilikombolewa kutoka kwenye ugaidi na operesheni ya amani ya spring, Oktoba 13, mwaka 2019.

Kundi la kigaidi la YPG / PKK, ambalo linaendelea na kazi yake, mara nyingi huandaa mashambulizi ya kigaidi kwa kulenga maeneo ya Rasulayn na Tal Abyad ambayo yamekombolewa kutoka kwenye ugaidi na operesheni ya amani ya spring. **TRT**

## Wanajeshi waondoka kwa Bobi Wine

**Kampala,** UGANDA

WANAJESHI waliokuwa wameyazingira makazi ya kiongozi wa upinzani nchini Uganda, Robert Kyagulanyi maarufu Bobi Wine, wameondoka kwenye makazi hayo.

Jumatatu, Mahakama iliamuru jeshi na polisi kuondoka kwenye makazi yake. Awali jeshi lilisema kuwa litatii uamuzi wa Mahakama.

Bobi Wine hakutoka kwenye makazi yake yaliyo kando ya mji wa Kampala, tangu alipopiga kura kwenye uchaguzi mkuu wiki mbili zilizopita.

Hata hivyo, aliandika katika ukurasa wa twitter kuwa jeshi bado linawazuia wageni wake.

Waandishi wa habari wa gazeti la Daily Monitor walisema, jeshi na polisi walikuwa wameimarisha ulinzi kwenye barabara inayoelekea kwenye makazi ya Bobi Wine na vituo vya ukaguzi vimeongezeka.

Magari mawili yaliyokuwa yamewabeba waandishi wa habari kuelekea nyumbani kwa Bobi Wine, walizuiwa na kuamriwa kurejea walikotoka.

Bobi Wine, majira ya mchana alitoka nyumbani kwake kwenda kuzungumza na vyombo vya habari, Daily Monitor la Uganda liliripoti. **BBC**

## Biden aruhusu waliobadili jinsia jeshini

**Washington,** MAREKANI

RAIS Joe Biden ameondoa katazo lililowekwa na Donald Trump la kuwapiga marufuku watu waliobadili jinsia kujiunga na jeshi.

Marufuku hiyo ilitangazwa na Trump mwaka wake wa kwanza akiwa Rais wa Marekani.

"Watumishi waliobadili jinsia hawatakabiliwa na uwezekano wa kuondolewa au kutengwa kwa misingi ya utambulisho wao kijinsia," ilisema ikulu ya White House.

Kulikuwa na askari 8,980 mwaka 2019, kwa mujibu wa takwimu za Idara ya Ulinzi zilizochambuliwa na Taasisi ya Palm Center.

"Rais Biden anaamini kuwa jinsia haipaswi kuwa kikwazo kwenye utumishi jeshini, na kuwa nguvu ya Marekani iko kwenye utofauti wake," taarifa ya Ikulu iliongeza.

Waziri mpya wa Ulinzi Lloyd Austin, Jenerali wa Jeshi mstaafu, alisema kwenye taarifa: Idara itatumia sera hii kuhakikisha kuwa watu wanaojipambanua kuwa wamebadili jinsia wanapata uhalali wa kuingia na kutumikia jeshi.' **BBC**




# DZEKO AKATAA KUTUA WEST HAM

**ROME,** Italia

WAKALA wa Edin Dzeko, amesema mshambuliaji huyo wa Roma amekataa kuhamia klabu ya West Ham inayoshiriki Ligi Kuu England.

Urafiki kati ya nahodha huyo wa Roma na kocha, Paulo Fonseca ulivunjika na mshambuliaji huyo pia hakujumuishwa kwenye orodha ya kikosi cha 'Giallorossi' hao kilichowakabili Spezia wikiendi iliyopita.

Dzeko alifanya mazoezi kando na wachezaji wengine na Sky Sport ikiripoti kuwa Roma hakupata klabu yoyote inayovutiwa na huduma ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34.

Lakini kwa mujibu wa gazeti la Calciomercato, West Ham waliwasilisha ofa ya kumsajili mshambuliaji huyo wa zamani wa Manchester City.

Hata hivyo, Dzeko amekataa ofa ya 'Wagonga Nyundo' - West Ham, lakini anasisitiza kuwa anataka kuondoka dimbani pale Olimpico katika dirisha hili la Januari.

# Ozil: Arsenal itabaki moyoni mwangu

**ISTANBUL,** Uturuki

MESUT Ozil amesema daima ataipenda na kuithamini klabu ya Arsenal, licha ya kuondoka klabuni hapo na kujiunga na Fenerbahce ya Uturuki.

Ozil ametoa kauli hiyo kupitia barua ya wazi aliyoianika kwenye mitandao ya kijamii, baada ya kusaini mkataba wa miaka mitatu na nusu kuitumikia Fenerbahce, ambayo imemsajili kwa uhamisho huru, kufuatia makubaliano yaliyofikiwa kati ya mchezaji huyo na viongozi wa Arsenal.

Kiungo huyo mwenye umri wa miaka 32, amesema akiwa Arsenal alicheza kwa heshima na kuipenda klabu hiyo na mwishowe alifanikiwa kutwaa taji la FA mara tatu, huku akifunga mabao 44 katika michezo 254 kwenye michuano yote aliyocheza.

"Ni vigumu kwangu kuweka kwa maneno upendo ninaohisi kwa klabu na mashabiki," alisema Ozil kupitia barua hiyo.

"Ninawezaje kuelezea miaka minane ya shukrani kwa barua moja? Nitakuwa Arsenal kwa maisha yote bila shaka juu ya hilo.

Ozil alijiunga na 'Washikabunduki' hao akitokea Real Madrid kwa pauni milioni 42.4 mwaka 2013 ikiwa ni ada ya uhamisho wa rekodi ya klabu hiyo na akaanza vizuri waliposhinda Kombe la FA msimu wake wa kwanza akimaliza kusubiri kombe kwa miaka tisa.

Alicheza michezo 32 msimu wa 2014-15, licha ya kukosa miezi mitatu kutokana na jeraha la goti, na akashinda Kombe la FA kwa mwaka wa pili mfululizo.

Alikuwa pia mchezaji wa kwanza kutengeneza bao katika michezo sita mfululizo na aliteuliwa kuwa mchezaji bora wa msimu kwa Arsenal.

Alikuwa mchezaji anayelipwa mshahara mkubwa zaidi katika historia ya klabu hiyo na mnamo Januari 2018, akisaini mkataba mpya wa miaka mitatu na nusu akilipwa takriban Pauni 350,000 kwa wiki.






# Mourinho: Kutimuliwa kwa Lampard ni ukatili

**LONDO,** England

KOCHA wa Tottenham Hottspur, Jose Mourinho, anaamini kwamba, kitendo cha Chelsea kumfukuza Frank Lampard ni ukatili katika soka la kisasa.

Chelsea juzi ilimtimua Lampard baada ya miezi 18 ya kuwanoa 'The Blues' hao wenye maskani yao pale Stamford Bridge jijini London.

Mouriho ambaye aliwahi kumnoa Lampard wakati akifundisha pale Chelsea kwa vipindi viwili tofauti, amesema Lampard hakupaswa kufukuzwa sasa, kwani alikuwa anahitaji muda.

"Nimehuzunishwa kwa kushindwa kwa kwao kumpa muda wa kutosha afanye mengi mazuri yenye mafanikio," alisema Mourinho akinukuliwa na BT Sport.

"Siku zote sifurahii mwenzangu kupoteza kazi. Frank sio tu nimewahi kufanya naye kazi, bali ni mtu muhimu kwenye kazi yangu, kwa hiyo namuonea huruma kufukuzwa kwake."

Maoni ya Mourinho yanajiri baada ya juzi kujihakikisha ushindi wa mabao 4-1 dhidi ya Wycombe Wanderes unaowapeleka raundi ya tano ya Kombe la FA ambapo sasa watakutana na Everton katika Uwanja wa Goodson Park Februari 10, mwaka huu.

## HABARI MICHEZO

# Corona yamkimbiza Benitez Ligi Kuu China

**MADRID,** Hispania

ALIYEKUWA kocha wa klabu za Liverpool, Newcastle United na Real Madrid, Rafael Benitez, ameachia ngazi kama Kocha Mkuu wa Klabu ya Dalian Professional inayoshiriki Ligi ya China, kwa makubaliano na viongozi wa klabu hiyo.


Kocha huyo kutoka nchini Hispania alikuwa amesajiliwa na mkataba wa mwaka mmoja, huku akilipwa mshahara wa pauni milioni 12 kwa mwaka, ambapo alianza kufanya kazi Julai 2019, muda mfupi baada ya kuondoka Newcastle United.

Benitez mwenye umri wa miaka 60, amesema amefanya uamuzi huo kwa sababu ya wasiwasi juu ya afya na ustawi wa familia yake wakati huu wa janga la corona.

Hata hivyo, habari hizi huenda zitawavutia sana mashabiki wa Newcastle United, ambao wanamkubali Benitez kutokana na mafanikio ya miaka mitatu pale St James 'Park kati ya mwaka 2016 na 2019.

Mashabiki wa Newcastle United wamechoshwa na kocha wao wa sasa, Steve Bruce kutokana na mambo kuwaendea kombo kwenye michezo ya Ligi Kuu, huku wakiwa wameshatolewa kwenye michuano ya Kombe la FA.

Benitez ni miongoni mwa makocha wanaopendekezwa kuchukua nafasi ya Bruce endapo wataamua kufanya mabadiliko kwenye benchi la ufundi katika kipindi hiki.






# MCKENNIE KUKAMILISHA UHAMISHO JUVENTUS

**TURIN,** Italia

WESTON McKennie anatarajiwa kukamilisha uhamisho wa kudumu wa pauni milioni 18.5 kwenda Juventus katika msimu wa majira ya joto.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, alijiunga na Bianconeri hao kutoka Schalke 04 kwa mkataba wa mkopo wa euro milioni 4.5 msimu wa joto uliopita.

Makubaliano hayo yalikuja na chaguo la kufanya uhamisho wa kudumu wa nyota huyo kwa dau la euro milioni 18.5.

Kwa mujibu wa Sky Sport Italia, Juventus itakuwa na jukumu la kumnunua mchezaji huyo moja kwa moja kama watamaliza katika nafasi nne za juu kwenye msimamo Ligi Kuu.

Hata hivyo, Juventus wako wazi kumsaini McKennie bila kujali kipengele kinachowalazimisha kumnunua.

Ada ya mwisho ya uhamisho wa McKennie kwenda Juventus inaweza kufikia euro milioni 30 na nyongeza.

Nyota huyo wa zamani wa Schalke 04, McKennie ana mabao manne katika mechi 21 kwenye mashindano yote hadi sasa msimu huu.

# *Lampard aishukuru Chelsea akitimuliwa*

**LONDON,** England

BAADA ya kufutwa kazi ndani ya Chelsea, Frank Lampard, amesema ilikuwa ni heshima kwake kuwa kocha ndani ya timu hiyo, hivyo anashukuru kwa yote.

Lampard alifutwa kazi Januari 25 na taarifa rasmi ilieleza kuwa ulikuwa ni uamuzi mgumu ambao mmiliki na Bodi ya Chelsea haikutaka kuufanya kwa kuwa matokeo hayakuwa bora hivi karibuni.

Alitangazwa kuwa kocha ndani ya timu hiyo Julai 4, mwaka jana na amekiongoza kikosi hicho kwenye jumla ya mechi 84 na anaondoka timu ikiwa nafasi ya tisa na pointi zake 29 kibindoni.

Inaelezwa kuwa anayetajwa kubeba mikoba ya Lampard ndani ya Chelsea ni Thomas Tuchel ambaye alikuwa kocha ndani ya Klabu ya PSG ila alifutwa kazi kutokana na matokeo mabovu.

Lampard amesema: "Kwa muda mrefu nimekuwa ndani ya Chelsea ila ninafurahi kufanya kazi hapo, ninapenda kuwashukuru mashabiki kwa sapoti ambayo wamenipa kwa muda wa miezi 18.

"Uongozi pia na wote ambao wamekuwa pamoja nami, ninajua kwamba changamoto ni jambo ambalo haliepukiki, ila kwa kushindwa kufikia mafanikio kwangu ni maumivu, ninaushukuru uongozi kiujumla na kila mmoja, nawatakia mafanikio mema."



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MADRID YAONGEZA KASI KUMNG'OA MBAPPE PSG

●●● Hata hivyo, Liverpool nao wameonyesha nia ya kutaka kumsajili mchezaji huyo ili...

**MADRID,** Hispania

KYLIAN Mbappe ametawala kurasa za mbele za magazeti ya jana Jumanne ya Diario AS na Mundo Deportivo, wakati Real Madrid ikijaribu kutaka kumsajili nyota huyo wa Paris Saint-Germain.

Mbappe mkataba wake wa sasa unamalizika mwaka 2022 na amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka kwa mabingwa hao wa Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, PSG kwenda kwa mabingwa wa LaLiga, Real Madrid mwishoni mwa msimu huu.

Kwa muda mrefu Real Madrid wamekuwa wakihusishwa na Mbappe, lakini sasa wanaonekana hawafanyi mzaha hata kidogo, kwani wana nia ya dhati kabisa ya kutaka kumpeleka pale kwenye dimba la Santiago Bernabeu.

**Kwa mujibu wa magazeti hayo, Mbappe ameripotiwa kuwa yupo tayari kwenda kwa miamba hao yenye maskani yao Mji Mkuu wa Hispania, Madrid.**

Hata hivyo, Liverpool nao wameonyesha nia ya kutaka kumsajili mchezaji huyo ili kuimarisha kikosi chao.

Wakati mlipuko wa virusi vya corona unaonekana umeathiri soko la usajili barani Ulaya, lakini Madrid wamejipanga kumchukua Mfaransa huyo usajili ambao unaweza kumhusisha na Vinicius Junior kwenda upande wa pili.

Gazeti la Mundo Deportivo limesema mabingwa wa Ligi Kuu ya England, Liverpool nao wapo tayari kuvunja benki kumsajili Mbappe.

Mbappe ndiye mchezaji anayetajwa kuwa na thamani kubwa zaidi kwa sasa duniani na dau lake la kwenda pale Madrid linaweza kuwa kubwa sana.

## ZISIKUPITE

### DZEKO KUONDOKA ROMA

EDIN Dzeko anatarajiwa kuondoka klabu ya AS Roma baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34 raia wa Bosnia, kutofautiana na kocha, Paulo Fonseca. ***(Goal)***

### LINGARD HUYOOO WEST HAM

KOCHA wa West Ham, David Moyes, anamtaka kiungo wa kati wa Manchester United, Jesse Lingard, baada ya bosi wa 'Mashetani Wekundu', Ole Gunnar Solskjaer kukubali kumruhusu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, kuondoka kwa mkopo. ***(Evening Standard)***

### VERON AWINDWA ULAYA

MANCHESTER United ipo kwenye mbio moja na Manchester City, Barcelona na Juventus, kuwania saini ya mchezaji mwenye umri wa miaka 18 raia wa Brazil, Gabriel Veron kutoka Palmeiras. ***(Sport via Star)***

### UNITED YAMFUNGUKIA VAN DIJK

MCHEZAJI wa zamani wa Southampton, Charlie Austin mwenye umri wa miaka 31, amesema kwamba Manchester United iliamua kumsajili beki wa Sweden, Victor Lindelof mwenye umri wa miaka 26, badala ya beki wa Liverpool na Uholanzi, Virgil van Dijk mwaka 2017. ***(Talksport)***

### LIVERPOOL KUMSAJILI GORDON

LIVERPOOL inakaribia kuafiki makubaliano ya dau la pauni milioni moja kumsajili kinda wa klabu ya Derby, Kaide Gordon mwenye umri wa miaka 19. Mchezaji wa timu ya Taifa ya England chini ya umri wa miaka 16, amehusishwa na uhamisho kuelekea Man United na Tottenham. ***(Liverpool Echo)***

### MUSTAFI ATETA NA ARSENAL

SHKODRAN Mustafi mwenye umri wa miaka 28, ameanza mazungumzo na Arsenal kuhusu kukamilisha mkataba wake mapema. Mchezaji huyo wa Ujerumani amehusishwa na uhamisho wa kuelekea klabu ya Lazio na beki huyo pia amekuwa akivutia klabu za Ujerumani. ***(Football London)***

### POCHETTINO AMTAKA DELLE

KOCHA wa Paris St-Germain, Mauricio Pochettino, anatarajia kujiunga tena na kiungo wa kati Delle Alli. Maombi matatu ya mabingwa hao wa Ufaransa kutaka kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, yamekataliwa lakini Pochettino anaungwa mkono na klabu hiyo kuendelea kumnyatia. ***(The Athletic)***

### PSG KUMBADILISHA DRAXLER

KLABU ya PSG imeripotiwa kumtoa kiungo wa kati wa Ujerumani, Julian Draxler, mwenye umri wa miaka 27, kama mbadala wa mchezaji wa Arsenal na Ufaransa mwenye umri wa miaka 21, Matteo Guendouzi. ***(L'Equipe via Mirror)***

### UDINESE YAMTAKA CUTRONE

KLABU ya Udinese ipo katika mazungumzo na klabu ya Wolves ili kumsajili kwa mkopo mchezaji wa Italia, Patrick Cutrone, mwenye umri wa miaka 23. Mshambuliaji huyo amekuwa hachezeshwi pale kwenye Uwanja wa Molineux tangu kuwasili kwa Willian Jose kutoka klabu ya Real Sociedad. ***(Express & Star)***

## Ufaransa waja na tamasha la Pamoja

**Na Faustine Feliciane**

UBALOZI wa Ufaransa nchini kwa kushirikiana na baadhi ya wasanii hapa wa Tanzania wameandaa tamasha kubwa la muziki na sanaa ya uchoraji lililopewa jina la 'Pamoja' litakalofanyika kesho kwenye viwanja vya Alliance de France.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijjni Dar es Salaam, Balozi wa Ufaransa nchini, Fredric Claver, alisema lengo la tamasha hilo ni kuimarisha ushirikiano wa nchi za Tanzania na Ufaransa na kudumisha tamaduni za nchi hizo.

Balozi huyo alisema Rais wa Ufaransa, Emmanuel Macron, amekuwa na nia ya dhati ya kujenga upya uhusiano mzuri baina ya nchi yake na nchi nyingine za Afrika ikiwamo Tanzania.

Tamasha hilo mbali na kuhusisha muziki wa asili pia litahusisha sanaa ya uchoraji kutoka kwa wasanii wa Tanzania na nje ya nchi.

Mmoja wa wasanii wa muziki kutoka bendi ya Bahati, Pili Maguzo, aliwataka Watanzania kujitokeza kwa wingi kesho kushuhudia tamasha hilo.

## Polisi kufuta uteja ikiivaa Mlandege leo

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Polisi Zanzibar imepanga kufuta uteja wa kupoteza mechi za Ligi Kuu Zanzibar, itakapokutana na Mlandege kwenye mchezo wa ligi hiyo leo.

Akizungumza na gazeti hili Kocha wa timu ya Polisi, Yusuph Sape, alisema timu yake kwa sasa imejipanga kuhakikisha inapata ushindi katika mechi zake zote za nyumbani na hata za ugenini ili kujiweka salama katika msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 12.

"Mwanzo tulikuwa tunafungwa na kupoteza nafasi nyingi, kama mwalimu nilijitathmini na kujua kwamba tatizo lipo kwa washambuliaji na hata mabeki maana wakati mwingine unaona washambuliaji wakipoteza nafasi ya wazi kabisa na hii inatokana na kutokuwa makini langoni, jambo ambalo tumelifanyia maboresho," alisema.

Leo itapigwa michezo miwili ya ligi hiyo ambapo katika Uwanja wa Mau A, Polisi itaumana na Malandege wakati katika Dimba la Amaan timu ya Malindi ivaana na Zimamoto.

# YANGA MAZOEZINI BILA NTIBAZONKIZA, YACOUBA

**Na Adam Fungamwangwo**

MABINGWA wa Kombe la Mapinduzi, Yanga, juzi walianza rasmi mazoezi kujiandaa na mechi za mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara bila baadhi ya nyota wao.

**Yanga ilianza mazoezi Kigamboni, ikiwa na mchezaji wake mpya, Dickson Job, iliyomsajili kipindi cha dirisha dogo akitokea Mtibwa Sugar, lakini ikiwakosa nyota wake wawili Saidi Ntibazonkiza na Yacouba Sogne ambao ni majeruhi.**

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Cedric Kaze amesema wameanza mazoezi baada ya siku 10 za mapumziko, hivyo anachofanya ni kuwarejesha wachezaji wake kwenye hali ya kupambana.

"Leo [juzi] ni siku ya kwanza baada ya mapumziko ya siku 10. Tunaangalia ni vitu gani tuanze navyo na mazoezi ya aina gani ili kwenda kwenye mechi za Ligi Kuu kwa sababu mzunguko wa pili unakuwa na ushindani wa hali ya juu," alisema Kaze.


Alisema ana imani baada ya siku chache wachezaji wake watakuwa wamerudi kwenye viwango vyao vya kawaida, pamoja na muunganiko kabla ya kuanza kwa ligi, lakini hata hivyo akisema kuwa bado ana baadhi ya wachezaji ambao ni majeruhi na hawajaanza mazoezi.

"Yacouba na Saido bado ni majeruhi, lakini tuna imani wiki hii wanaweza kuwa sawa. Lakini kuna wachezaji wangu ambao wako kwenye kikosi cha timu ya taifa nao bado hawajajiunga na timu, natumai kikosi kikikamilika mambo yatakwenda vizuri," alisema kocha huyo wa vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa.

Naye mchezaji mpya wa kikosi hicho, Job, alisema amefurahi kujiunga na timu hiyo na ni siku yake ya kukumbukwa kwa kuanza rasmi mazoezi akiwa na mabingwa hao wa kihistoria.

"Ilikuwa ni ndoto yangu siku moja nicheze moja ya klabu kubwa Tanzania, na kweli leo nimekuwa na furaha kwa sababu nimetua Yanga," alisema.

Alisema kuwa hana wasiwasi na amejipanga kuonyesha uwezo wake wote na kile ambacho kilisababisha Yanga wamuone na kumsajili.




Mshindi wa bonasi ya Jackpot, Colonel Keyu (katikati), akikabidhiwa mfano wa hundi yenye thamani ya Sh. milioni nane na wachezaji wa timu zinazodhaminiwa na SportPesa, winga Hassan Dilunga wa Simba (kushoto) na kiungo Haruna Niyonzima wa Yanga. Mshindi huyo alibashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya 13 kwenye Jackpot ya SportPesa. Jackpot ya SportPesa sasa imefikia dau la Sh. 426,664,100 kwa atakayefanikiwa kubashiri kwa usahihi mechi zote 13. **PICHA: SPORTPESA**

# *Pambano la Class, Mwale lapamba moto*

**Na Mwandishi Wetu**

BODI ya Utalii Tanzania (TTB), imesema itatumia pambano la bondia Ibrahim Class na Dennis Mwale wa Zambia (Rhumbo in Dar) kuutangaza utalii wa nchi za nje ya mipaka yake.

Bondia wa Tanzania, Class na Mwale watapambana Ijumaa kwenye ukumbi wa Next Door Arena, Masaki jijini Dar es Salaam kuwania ubingwa wa mabara wa WBF wa uzito wa Super Feather.

Pambano hilo limeandaliwa na Kampuni ya Jackson Group Sports na litaonyeshwa nchi zaidi ya 150 duniani. Siku hiyo pia kutakuwa na mapambano mengine nane yakishirikisha mabondia mbalimbali ikiwa ni pamoja na bondia nyota wa Bulgaria, Tervel Pulev ambaye ameshawasili pamoja na bondia nyota wa uzito wa juu duniani Kubrat Pulev ambaye alipigana na Anthony Joshua mwishoni mwa mwaka jana.

Mkurugenzi wa Masoko wa TTB, Mindi Kasiga alisema jana kuwa watatumia fursa hiyo kutangaza utalii wa nchi kwani mapambano hayo ya ngumi yataonekana nchi nyingi.

"Hii ni fursa kwetu kuutangaza utalii na kuingia kusapoti Jackson Group Sports," aliema Kasiga.

Mbali ya TTB, pambano hilo limedhaminiwa na Benki ya CRDB ambapo meneja wa chapa, Joe Bendera, alisema wanazidi kuendeleza michezo nchini kwani walidhamini pia mpira wa kikapu, kuandaa marathon na kutoa fursa ya masomo kwa vijana 26 kupitia mpira wa kikapu.

Kwa upande wa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Global Boxing Stars (GBS), Scott Farrell, alisema wamevutiwa na Kampuni ya Jackson Group Sports na kuamua kufanya nao kazi pamoja kuinua mchezo wa ngumi za kulipwa.

Alisema lengo lao ni kuinua vipaji vya mchezo huo hapa nchini. Mbali ya wadhamini hao, wadhamini wengine ni Azam TV, Onomo Hotel, Precision Air, Vitasa, Bono 5, Hotel Demag na Henessy.

Mkurugenzi Mtendaji wa Jackson Group Sports, Kelvin Twissa, alisema maandalizi ya pambano hilo yamekamilika na mabondia wote wamewasili kwa ajili ya kuzichapa Ijumaa, huku akifafanua kuwa kila mabondia wote wana ari kubwa ya kushinda katika pambano hilo.

Michezo
Jumatano Januari 27, 2021
Nipashe



Madrid yaongeza kasi kumng'oa Mbappe UKURASA 22

# GOMES AKUNWA NA CHIKWENDE, KAHATA

## Wakati wakiivaa Al Hilal leo, vipaji Simba vyampagawisha, amtaja...

**Na Saada Akida**

WAKATI leo akikiongoza kwa mara ya kwanza kikosi cha Simba kwenye mechi ya kwanza, watakaposhuka dimbani kuvaana na Al Hilal ya Sudan katika mashindano ya Simba Super Cup, Kocha Mkuu wa Mabingwa hao wa Tanzania Bara, Mfaransa Didier Gomes, amesema mazoezi waliyofanya pamoja na wachezaji wa timu hiyo kwa muda wa siku mbili, yamempa mwanga mzuri wa kuwajua nyota wake.

**Mashindano hayo yaliyoandaliwa na Simba ambayo yatafanyika katika Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam yakishirikisha timu tatu nyingine ikiwa ni TP Mazembe ya DR Congo, ni maalum kwa ajili ya kujiandaa na mechi za hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika ambapo klabu hizo tatu zimetinga hatua hiyo, lakini zipo makundi tofauti.**

Akizungumza na Nipashe, Gomes amesema michuano hiyo itampa mwanga zaidi wa kutambua wachezaji wake na kujenga kikosi imara kuelekea Ligi Kuu Bara, Kombe la Shirikisho pamoja na Ligi ya Mabigwa Afrika. Nipashe lilipotaka kujua hadi sasa katika mazoezi ya siku mbili ni wachezaji gani wameonyesha kumvutia, Gomes alisema amekunwa na uwezo wa viungo, Clatous Chama, Francis Kahata pamoja na mshambuliaji Meddie Kagere huku akiisifu Simba kwa usajili mzuri wa Perfect Chikwende.

"Nimemuona Chikwende, ni mchezaji mzuri sana, mzuri kiufundi, ni mwenye hisia nzuri za uchezaji, jana (juzi) pia niliona wachezaji wapya waliojiunga nasi kama Kahata, Chama na Kagere ni wachezaji wazuri na muhimu kuwapo katika timu," Gomes alisema.

Gomes alisema anatambua kwamba ana kazi kubwa ya kufanya kuhakikisha wachezaji wa timu hiyo wanakuwa na umiliki mkubwa wa mpira pamoja na kushambulia kwa kasi, hivyo anaamini uwezo na vipaji walivyonavyo utamwezesha kufikia malengo yake.

"Nimevutiwa na wachezaji kuanza kuelewa nataka mchezo wa kasi, lakini Simba Super Cup ni mashindano mazuri kwetu na wanaokuja kushiriki, kwangu yananipa nafasi ya kuwatambua zaidi wachezaji wangu ili kujenga kikosi imara," alisema Gomes.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa Al Hilal ya Sudan, Zoran Manojlovic, amesema mashindano ya Simba Super Cup ni moja ya maandalizi muhimu kwao kuelekea kujiandaa Ligi ya Mabingwa Afrika.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Zoran alisema itakuwa sehemu nzuri kwao kupata mazoezi kutokana na timu zinazoshiriki ni miongoni mwa zilizofuzu Ligi ya Mabingwa hatua ya makundi.

"Itakuwa ni maandalizi mazuri kwetu lakini tumekuja kushindana, tutaleta ushindani kuhakikisha tunarejea na kombe nyumbani," alisema Zoran.

Mratibu wa mashindano hayo kutoka Shirikisho la Soka Tanzania, Baraka Kizunguto, alisema: "Hii lazima bingwa apatikane, kama timu zote zitalingana pointi, tutaangalia mabao ya kufunga na kufungana, walipokutana, kama zote zimefanana basi tutaangalia nani aliyeanza kufunga mwisho ni kuangalia nidhamu ya timu kuangalia kadi za njano," alisema Kizunguto.

Alisema katika mashindano hayo kutakuwa na mchezaji bora, mfungaji bora na kipa bora, ambao watazawadiwa medali na kikombe kikitolewa kwa bingwa.

Katika hatua nyingine, Klabu ya Simba jana imetangaza kumsajili beki wa kati wa Highlanders FC ya Zimbabwe, Peter Muduhwa, aliyekuwa Cameroon na kikosi cha timu ya Taifa ya Zimbabwe kilichokuwa kikishiriki Fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani, CHAN.

"Karibu kwenye familia kubwa ya mabingwa wa nchi beki kisiki, Peter Muduhwa (Master of Defense). Wanasimba tunakupokea kwa mikono miwili na tunaamini utatufanyia kazi kubwa katika michuano ya Ligi ya Mabingwa na Simba Super Cup," ilieleza taarifa ya Simba jana.

**BEKI KISIKI...**



Beki mpya wa kati wa Simba kutoka Highlanders FC ya Zimbabwe, Peter Muduhwa, akitia saini mkataba wa kuwatumikia mabingwa hao wa Ligi Kuu Bara jana. **PICHA: SIMBA**

## Stars yaapa kufia uwanjani

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA Mkuu na Nahodha wa Taifa Stars, Etienne Ndayoragije na John Bocco, wamesema watafanya kila linalowezekana ili kushinda mechi ya leo dhidi ya Guinea na kutinga robo fainali ya Fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), kwenye michuano hiyo inayoendelea nchini Cameroon.

Wakizungumza nchini Cameroon jana, kocha na nahodha huyo wamesema wanaamini kuwa watafanya vema kutokana na ari ya wachezaji wa kikosi hicho, hasa baada ya kupata ushindi kwenye mechi ya pili dhidi ya Namibia kwa bao 1-0.

"Maandalizi yako sawa. Hakuna majeruhi, vijana wana ari na tumewajenga kisaikolojia na tunajua umuhimu wa mechi. Tunakwenda kujitoa kwa sababu tunataka kufanya vizuri na kufikia malengo tuliyojiwekea.

"Tumejiandaa kwa vyote. Hatuwezi kusema tunashambulia tu, au tutazuia tu, tunafanya vyote kwa pamoja, ingawa timu yetu bado inaendelea kujijenga siku hadi siku, lakini tunatarajia kuwa bora kuliko mechi mbili za mwanzo," alisema Ndayiragije.

Kwa upande wa nahodha, Bocco alisema: "Tulipoteza mechi ya kwanza, lakini ya pili tulishinda. Tumerekebisha makosa tuliyoyafanya, tuna imani kuwa tutacheza kwa nguvu na kujituma ili kushinda na kuingia hatua ya robo fainali."

Stars inaingia uwanjani ikiwa na pointi tatu kwenye Kundi D, ikichapwa mabao 2-0 dhidi ya Zambia na ikashinda 1-0 dhidi ya Namibia huku Guinea na Zambia zote zina pointi nne, hivyo ni ushindi tu ambao utaihakikishia Stars kutinga hatua hiyo na si vinginevyo.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042